

Utajiri wa Watu Maskini



Muhtasari katika lugha rahisi kuhusu

MPANGO WA KURASIMISHA

RASILIMALI NA BIASHARA ZA WANYONGE

TANZANIA

MKURABITA

Februari 2007

Utajiri wa Watu Maskini

Muhtasari katika lugha rahisi kuhusu

MPANGO WA KURASIMISHA RASILIMALI NA BIASHARA ZA
WANYONGE TANZANIA –

MKURABITA

M K U R A B I T A

Shukrani

Kufuatia utangulizi waharakati za MKURABITA, watu wengi waliona umuhimu wa kuandaa taarifa ya lugha rahisi kuhusu MKURABITA ya kuwapatia taarifa watanzania wengi kuufahamu MKURABITA. Tunatumaini kuwa “Utajiri wa Watu Maskini” utawezesha idadi kubwa ya watu kuuchanganua na kuujadili MKURABITA kwa njia zinazokubalika.

“Utajiri wa Watu Maskini” umeandaliwa kwa msaada wa watu wengi. Kwanza kabisa shukrani zinastahil kwenda kwa Norwegian People’s Aid na Royal Norwegian Embassy, kwa kuufadhili mradi huu. Aidha shukrani ziende kwa kitengo cha usimamizi wa programu ya MKURABITA kwa kutoa waraka wa Programu ya MKURABITA. Sehemu ya 1 ya taarifa hii, imetokana na nyaraka hizi.

Shukrani za kipekee ziende kwa washiriki wa warsha za kupashana habari kuhusu MKURABITA zilizofanyika katika miji ya Dar Es Salaam na Arusha, kati ya mwezi Oktoba na Novemba 2006, pamoja na wote waliochangia maoni yao kwenye taarifa hii.

MKAKATI WA MKURABITA

Kuanzisha mfumo wa aina moja kitaifa wa haki za mali na biashara. Mfumo huu utatokana na uoanishaji maridhawa wa shughuli zilizozoeleka kuanzia chini kwenda juu pamoja na sheria zinazozihusu shughuli hizo kutoka juu kwenda chini.

LENGO LA MKURABITA

Kuwezesha vikundi na watu binafsi, hasa katika sekta isiyo rasmi, ili waweze kushiriki kikamilifu katika uchumi wa soko kisasa na rasmi.

SHABAHA YA MKURABITA

Kuwawezesha wanyonge walio wengi katika sekta isiyo rasmi waweze kutumia vizuri zaidi mali zao na rasilimali za biashara na kunufaika na fursa nyingine katika uchumi wa kisasa wa soko. Kwa hiyo, wataweza kupanua biashara zao, kuongeza kipato chao na kushiriki katika upunguzaji umasikini.

MATOKEO YANAYOTARAJIWA YA MKURABITA

Kupungua kwa umaskini katika ngazi ya kaya, kuinua ubora wa maisha ya kundi lengwa na kupanua uchumi wa taifa unaosimamiwa kisheria.

Yaliyomo

UTANGULIZI

SEHEMU YA KWANZA – Mpango Wenyewe 2

1. MKURABITA ni nini? 2

2. Kwa nini kurasimisha? 5

Misingi ya uchumi wa kisasa

nyenzo tatu za msingi za uchumi wa kisasa

hatua tatu za usalama na ushirikishwaji

Hatua kutoka sekta isiyo rasmi hadi sekta rasmi

Sekta ya kisheria – gharama za muda na fedha

Je, mabadiliko gani ni ya lazima?

3. Marekebisho ya MKURABITA – nini kinapendekezwa? 12

Rahisisha upatikanaji wa haki bayana za ardhi na uhamishaji wake.

Rahisisha uendeshaji wa biashara kisheria na kwa faida

Rahisisha upatikanaji wa mikopo na huduma nyingine za kifedha

Weka mfumo bora wa mawasiliano

4. MKURABITA – Majukumu na mahusiano 21

SEHEMU YA PILI– Maswali kuhusu MKURABITA 24

Maelezo

1 Maoni ya wadau kuhusu faida na hatari za MKURABITA 34

2 Marekebisho ya awali 37

3 Maandiko ya MKURABITA 39

4 Mahusiano ya Kimtandao 40

Hii ni tafsiri inayotumia lugha nyepesi inayohusu Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania ambao kwa Kiswahili ni maarufu kama MKURABITA. Tafsiri hii ina sehemu mbili.

Sehemu ya kwanza inaeleza kwa muhtasari mawazo makuu na matokeo yaliyopendekezwa ya programu ya MKURABITA. Haya yameelezwa katika sehemu ndogo nne. Kwanza, tunafafanua kwa ufupi maana ya MKURABITA. Tunachunguza dhana kwamba “Kurasimisha” rasilimali za Watanzania kutapelekea kupunguza umasikini, kwa kuwa kutawarahisishia watu kukopa.

Kisha tunachunguza kwa kina wazo zima kuhusu urasimishaji na namna utakavyochangia katika kupunguza umasikini. Tunaangalia seti za nyenzo tatu za kiuchumi zinazoweza kusaidia katika uchumi wa kisasa na tunatazama mchakato wa kujiondoa katika uchumi uliozoeleka usio rasmi kwenda katika uchumi wa kisasa ulio rasmi. Tunaangalia pia vikwazo vinavyowakabili Watanzania katika mfumo wa sasa wa kisheria na kirasimu, tunabainisha kwamba mchakato wa urasimishaji utakaoanisha mifumo ya sheria za kimila na za kisasa unaweza kuwarahisishia Watanzania kushiriki katika uchumi wa kisasa. Vilevile tunatazama masuala mengine ambayo ni lazima yatatuliwe ili maskini waweze kunufaika na mabadiliko haya ya urasimishaji.

Sehemu ndogo ya tatu ya Sehemu ya 1 inaonyesha baadhi ya marekebisho yaliyojadiliwa katika hatua ya sasa ya Programu ya Marekebisho ya MKURABITA. **Ili kuweza kushughulikia masuala haya, itabidi Serikali na Bunge kutoa uamuzi kuhusu mabadiliko yatakayofanyika katika sheria, taratibu na programu za serikali. Baadhi ya mapendekezo muhimu ya marekebisho yaliyopendekezwa hapa yanaweza kupitishwa na mengine yasipitishwe; baadhi yanaweza kutekelezwa mapema, na mengine yakachukua muda mrefu.** Sehemu ndogo ya mwisho inahusu baadhi ya uhusiano uliopo baina ya MKURABITA na programu nyingine na nani anawajibika katika utekelezaji wake.

Sehemu ya pili inajadili vipengele mbalimbali vya MKURABITA kwa kutumia maswali na majibu. Mambo mengi katika sehemu hii yamechukuliwa kutoka kwenye kumbukumbu za warsha za wadau.

Tafsiri hii inayotumia lugha nyepesi umebuniwa ili kuwasaidia wasomaji kuelewa zaidi kuhusu mada zile zinazowavutia zaidi. Kuna maelezo yaliyopo mwishoni mwa kurasa nyingi yakionyesha marejeo kuhusu MKURABITA yenye taarifa za kina kuhusu mada maalum. Vilevile kuna maelezo yaliyotolewa mwishoni mwa kijitabu hiki ambayo yanafafanua zaidi mawazo yasiyofafanuliwa kwa kina ndani ya kijitabu. Kwa msaada zaidi, wale wanaopenda kupata zaidi taarifa za kimataifa kuhusu MKURABITA wanaweza kuzipata taarifa hizo katika mtandao wa Intaneti.

... hakuna mkabala mmoja wa kuleta mabadiliko.

Changamoto kuu ni kubuni mkakati unaojali motisha na kutilia maanani hali changamani iliyoko katika kukabiliana na sekta isiyo rasmi kisheria, kijamii, kiutamaduni, kisiasa na kiuchumi – mkakati utakaozingatia uhusiano wa kutoka juu kwenda chini na kutoka chini kwenda juu, ukiakisi kikamilifu shabaha, vipaumbele, na mahitaji ya masikini; mkakati uliowazi, unaomilikiwa na wengi, na ambao mkabala wake utatekelezeka kwa ufanisi.
Tume ya Kiwango kuhusu Uwezeshaji Halali wa Masikini (Jan 2006) uk5

1. MKURABITA ni nini?

Katika sehemu hii tunaeleza kwa ufupi kuhusu MKURABITA. Tunachunguza wazo kwamba, “kurasimisha” rasilimali za Watanzania kutasaidia kupunguza umasikini, kwa kuwa kutawarahisishia watu kukopa na kuwekeza pindi rasilimali zao zitakapotambuliwa kisheria. Tunaweka bayana kuwa MKURABITA ni mpango changamani sana ambao upo katika awamu ya kuundwa na kwamba vipengele vingi kuhusu namna utakavyofanya kazi bado havijawekwa wazi.

Ingawa uchumi wa Tanzania umekuwa ukikua katika siku za hivi karibuni matokeo ya ukuaji huo wakati mwingine hayawafiki watu masikini katika jamii. Hii ina maana kwamba kasi ya upunguzaji umasikini bado hairidhishi.

Serikali ya Tanzania imeanzisha sera na programu kadhaa zenye lengo la kukuza uchumi na kupunguza umasikini kwa kupanua ushiriki wa Watanzania wote katika shughuli za kiuchumi.

Sera ya Uwezeshaji Kiuchumi ndiyo msingi wa juhudi hizo za Serikali. Sera hiyo ina lengo la kuwawezesha Watanzania kumiliki, kuendesha na kunufaika na uchumi wao wenyewe. Ili kufikia lengo hili, programu kadhaa zimeanzishwa kwa lengo la kuondoa baadhi ya vikwazo vinavyowakabili Watanzania katika shughuli za kiuchumi. Malengo mawili katika jumla ya malengo ya sera ya uwezeshaji ni kuboresha uwezo wa Watanzania katika kupata mikopo na kuboresha sheria na mifumo ya usimamizi ili iwanufaishe zaidi walengwa wake.

Moja ya mawazo ambayo Serikali inazingatia kama mbinu rahisi ya kupanua ushiriki katika uchumi ni kuwaingiza watu wengi zaidi katika uchumi rasmi na wenye kutumia kumbukumbu.



Vipi watu ambao hawana mali ya kurasimisha-masikini wa kutupwa? Watan ufaikaje?

Wazo la msingi hapa ni kwamba watu wengi masikini wanamiliki utajiri kama ardhi na biashara ndogondogo, lakini utajiri huu hautambuliwi kisheria, au 'haujarasimishwa'. Kama watu hawana hatimiliki ya ardhi yao, au wanafanya biashara ambazo hazijasajiliwa au zisizo na utaratibu wanaweza kukosa uwezo wa kupata mitaji au kupanua biashara zao nje ya mipaka yao. Hivyo, wazo kuu la

Ni aina gain ya mali MKURABITA inaziangalia zaidi?

Ni ardhi, nyumba na majengo mengineyo. Hata hivyo, maeneo mengine yanahusu mali zinazohamishika: Kwa mfano baiskeli, radio au gari ambayo inaweza kutumika kama dhamana ya kupata mkopo.

MKURABITA ni kuwezesha hili na kuwavutia watu masikini waweze kufanya kazi zao katika mfumo¹ rasmi, kisheria ili waweze kutumia rasilimali zao katika kukuza ushiriki wao sio tu kwenye soko la ndani bali pia katika soko la kitaifa na kimataifa. Lengo la msingi ni kupunguza umasikini.

Tunaposema biashara tunamaana aina zote za biashara: Mamalishe/Babalishe, mkulima mdogo anaye zalishe mazao ya biashara, biashara ndogo ndogo, ushirika au mashirika makubwa kuzalishe saruji.

Wazo kwamba kuwapa watu hatimiliki rasmi za mali na biashara zao kutaboresha nafasi zao kiuchumi limevuta sana usikivu kimataifa kupitia kazi ya mchumi mmoja wa huko Peru aitwaye Hernando de Soto². De Soto aliona kwamba masikini wengi duniani wana uchumi usio rasmi, ambao hautambuliwi na sheria ya nchi husika. Anaona kwamba sekta isiyo rasmi ni kikwazo cha maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa sababu katika mazingira ya namna hiyo watu huwa hawana haki na ulinzi wa kisheria wa kutosha, hivyo huwa hawana nguvu za kujitetea. Aliyekuwa rais wa awamu ya tatu wa Tanzania, Mh. Mkapa alimkaribisha Hernando de Soto kulihutubia Bunge la Tanzania mwezi Februari 2003. Kutokana na tukio hilo, Taasisi ya de Soto ya Haki na Demokrasia ilipewa jukumu la kuandaa Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania, maarufu kwa Kiswahili kama MKURABITA. MKURABITA unaandaliwa kwa hatua:

Tathmini ya Hali Halisi
(iliyoishia Oct 2005)

Hatua hii ilihusu tathmini ya hali halisi na ukubwa wa sekta ya nchi ya kisheria na ile isiyo rasmi pamoja na uchanganuzi wa faida na hasara za kubaki nje ya sekta ya sasa inayokubalika kisheria.

Muundo wa Marekebisho
(utakaishia Oct 2007)

Hatua hii itabainisha maelezo ya kina kuhusu sera na mkakati wa namna ya kuziingiza mali na biashara zisizo rasmi katika mfumo unaokubalika kisheria ili kuongeza ukuaji wa uchumi, kupunguza umasikini na hatimaye kupanua wigo wa kodi.

Utekelezaji³

Hatua hii itaendelea kwa miaka kadhaa na itatoa elimu kwa umma, na kutoa mafunzo kwa viongozi na kwa ujumla kuhakikisha kwamba marekebisho mbalimbali yanatekelezwa na kwamba mali iliyorasimishwa inaweza kutumika kuongeza utajiri, kutengeneza mtaji, na kupata maendeleo endelevu.

¹ Maelezo ya 1 yanaorodhesha baadhi ya maoni ya wadau kuhusu manufaa na hasara zinazoambatana na urasimishaji

² Mawazo yake yamendikwa kwenye vitabu viwili – “The Other Path” (1989) na “The Mystery of Capital – why capitalism triumphs in the West and fails everywhere else” (2000)

³ Waraka rasmi wa MKURABITA unataja hatua ya nne ‘Ukuaji Mtaji na Utawala Bora’, lakini katika hali halisi hili haliwezi kutengenishwa na utekelazaji

MKURABITA utakuwa ni mpango wenye changamoto kubwa sana katika utekelezaji wake. Ni muhimu kutambua kwamba mpango huu hauishii tu katika kurasimisha rasilimali za masikini. Bali pia una lengo la kuongeza uwezo na kiwango cha ujasiriamali nchini Tanzania ili kunufaika na uchumi uliorasimishwa. Mawanda yake yatahitaji uratibu mpana utakaojumuisha idadi kadhaa ya Wizara, Idara na mashirika ya Serikali. Aidha una madhumuni mengi yanayoendana na mipango mingine ya uwezesaji kiuchumi ya Serikali kama vile Mpango ya Kuimarisha Mazingira ya Biashara Tanzania (MKUMBITA), Mpango wa Kimkakati wa Kutekeleza Sheria za Ardhi (SPILL) na hasa MKUKUTA. Mpaka sasa bado haeleweki vyema namna ambavyo mpango huu utaoanishwa vilivyo na hizo programu nyingine

Kwa mujibu wa Taasisi ya Uhuru na Demokrasia, upo uwezekano wa kupatikana manufaa makubwa. Utafiti wa ubainishaji uliofanywa na Taasisi hii ulishauri kwamba Dola za kimarekani bilioni 29 zikiwa mitaji isiyotumika zilikuwa katika ardhi, rasilimali na biashara za sekta zisizo rasmi. Endapo kiasi hiki kikubwa cha mtaji kingeweza kutumika, Taasisi inabashiri kwamba kingeleta mabadiliko makubwa sana katika maisha 90% ya Watanzania ambao kwa sasa hawamo katika mfumo rasmi. Matarajio ni kukuza uchumi ambao kila mtu atanufaika, kama tu tungebainisha na kujifunza kutumia vizuri utajiri wa watu masikini. Hata hivyo, utafiti uliofanywa kwenye nchi zenye urasimishaji wa kiwango cha juu unapendekeza kwamba wakati watu masikini wangepata fursa ya kupata hakimiliki na usajili wa ardhi na biashara, wanaonekana kuwa hawataweza kuzitumia rasilimali hizi zilizorasimishwa kama dhamana kwa ajili ya kupata mikopo. Tutachunguza baadhi ya masuala haya baadaye katika taarifa hii.

2. Kwa nini Kurasimisha?

Katika sehemu hii tutachunguza zaidi wazo la urasimishaji na namna litakavyochangia katika kupunguza umasikini. Tutachunguza 'zana' tatu za kiuchumi zinazohitajika katika uchumi wa kisasa na katika hatua ya kutoka kwenye uchumi wa asili usio rasmi kwenda kwenye uchumi rasmi wa kisasa. Tunachunguza vikwazo vinavyowakabili Watanzania katika kushughulikia mfumo wa sasa wa kisheria na kirasimu. Mwisho tunabaini kuwa mchakato wa urasimishaji unaohusisha uanishaji wa mifumo ya sheria za kimila na za kisasa unaweza kuwarahisishia Watanzania kushiriki katika uchumi wa kisasa. Tunachunguza pia masuala mengine ambayo yanapaswa kutatuliwa ili kuwawezesha masikini kunufaika na urasimishaji.

Misingi ya Uchumi wa Kisasa

Katika mifumo ya kijadi ya uchumi watu hufanya biashara kwa kuaminiana kifamilia na kiurafiki, hivyo, huwa hakuna haja ya kuandikiana. Kwenye mfumo wa kisasa wa uchumi lipo tatizo la namna ya kushughulikia wageni hasa katika kubaini uaminifu wao. Nyaraka na taritibu zilizokubalika kisheria zinaweza kusaidia kudumisha kuaminiana kisheria na hivyo kudumisha ulinzi wa mali, manunuzi na malipo katika uchumi wa kisasa.

Historia inaonyesha⁴ kwamba kuna nyenzo tatu za msingi za uchumi ambazo zinapaswa kuwepo kama taifa linataka kuendelea na kuwa na mfumo wa uchumi unaomshirikisha kila mmoja. Nyenzo hizo ni (a) haki ya kumiliki mali, (b) hati muafaka za kuendeshea biashara na (c) nafasi katika soko kubwa. Tutajadili kila kimoja hapa. Kisha tutaangalia baadhi ya mambo ya nyongeza yanayohitajika katika nyenzo hizo tatu ili kuwawezesha watu masikini wanufaike nazo.



⁴ Tazama Hatua ya Mpango wa Marekebishi ya MKURABITA, Kiambatisho cha 1 kwa ajili ya kusoma kurasa 4 za ufupisho zilizoandikwa na Taasisi ya Uhuru na Demokrasia kuhusu mada hii

Jedwali la 1: Nyenzo tatu za uchumi

Nyenzo ya 1- Haki za kumiliki mali

Katika uchumi wa kisasa itaweza kuwasaidia watu ushahidi rasmi na maandishi yanayoonyesha kwamba wanamiliki ardhi na mali zao. Maandiko hayo si tu kwamba yanalinda umiliki wa mwenye mali bali pia yanaweza kutumika kama amana ya kupatia mkopo.

Nyenzo ya 2- Hati ya kuendeshea biashara

Katika uchumi wa kisasa wafanyabiashara mara nyingine wanaweza kunufaika wakiwa na hati halali ya kumtambua mmiliki. Mara kitambulisho hiki halali kinapopatikana, wageni watajisikia huru kufanya biashara zao. Biashara pia huhitaji kuwa na mgawanyo mzuri wa kazi na mikataba maalum ya ajira.

Nyenzo ya 3- Soko pana

Kwenye uchumi wa kisasa biashara hutafuta wateja na washirika katika viwango vya taifa na hata kiwango cha kimataifa. Hii huhitaji kuwa na nyaraka halali kisheria pamoja na hati za utambulisho ambazo zinaiwezesha biashara kuwa na mitandao salama, ya mawasiliano ya mahusiano na masoko ya mbali.

Unapofikiria kuhusu nyenzo hizi ni vizuri pia kuzitafakari katika hatua tatu ambazo huleta manufaa ya usalama kisheria na kuruhusu ushiriki katika masoko. Wazo lenyewe ni kwamba mara haki na hatimiliki zinapoandikwa⁵ zinaweza kusajiliwa katika ngazi ya juu na hii itasaidia katika kushughulika na wageni na hivyo kufanya biashara na rasilimali zako kukua. Hatua hizi zimeelezwa kwa ufupi katika jedwali hili hapa chini⁶.

Jedwali la 2: Hatua tatu za usalama na ushirikishwaji

Hatua ya 1- Umiliki

Haki za kumiliki mali, biashara pamoja na mikataba vinaweza kuandikwa rasmi kwa kutumia fomu maalum inayokubalika kisheria. Hivyo unaweza kutumia ‘mali’ zako kwa uhuru zaidi.

Hatua ya 2- Usajili

Nakala za nyaraka zinaweza kuwekwa kwenye rejesta rasmi (baadhi za ndani na nyingine za ngazi za juu – lakini zote zikiwa zinahusiana). Hapa rasilimali zako ni salama zaidi.

Hatua ya 3- Uingizaji sokoni

Mara uandikishaji na usajili unapokamilika na kurasimishwa basi mlango sasa uko wazi kwenye mifumo mipana zaidi ya taifa na masoko ya kidunia. Hii ina maana kwamba umuhimu wa kukua kwa biashara yako sasa unaonekana.

⁵ Istilahi ya sasa inayotumika kuelezea mchakato huu ni ‘ukaratasishaji’

⁶ Tazama maelezo ya 2 kwa ajili ya kupata mchanganuo wa masuala ya marekebisho ya awali yakiwa yamegawanywa kulingana na zana tatu za kisasa za uchumi na viwango vitatu vya usalama na ushirikishwaji.

Hatua kutoka sekta isiyo rasmi hadi sekta rasmi



Hivyo, wakati wa kutafakari kile ambacho MKURABITA unapendekeza ni muhimu pia kufikiria mkondo wa maendeleo kuanzia mfumo wa kijadi, usio rasmi kwenda mfumo wa kisasa usio rasmi hadi mfumo wa kisasa ulio rasmi. Jedwali lifuatalo linaorodhesha baadhi ya tofauti hizo.

Jedwali la 3: Kuelekea kwenye uchumi wa kisasa na rasmi

KIJADI		KISASA		Rasmi
		Ulimwengu wa hati na sheria - kushughulika na wageni		
Isiyo rasmi Dunia isiyotegemea maandiko - dunia ya kushughulika na familia na marafiki	→	Isiyo rasmi Nyaraka na rejesta za ndani	→	Rasmi Nyaraka na rejesta zilizo halali kisheria

Utafiti uliofanywa na Taasisi ya Uhuru na Demokrasia unaonyesha kwamba Watanzania wengi tayari wanaondoka kwenye njia za kusimamia ardhi na kuendesha biashara zao kijadi⁷. Wamebaini umuhimu wa kuwa na nyaraka pamoja na rejesta zitakazohifadhi vizuri nyaraka hizo. Hata hivyo, kama ingekuwa rahisi kwa watu kuingia moja kwa moja katika uchumi wa kisasa, basi wengi wangukuwa wameshafanya hivyo. Ukweli ni kwamba ni vigumu, hasa kiuwezo, kwa Watanzania wa kawaida kuendesha shughuli zao katika uchumi rasmi. Kwa hiyo, Watanzania wengi masikini zaidi hulazimika kutumia mifumo isiyo rasmi. Hii ni kwa sababu hawana uwezo, kimuda na kifedha, wa kutumia mifumo rasmi na halali kisheria ya kitaifa iliyopo. Aidha utafiti wa Taasisi ya Uhuru na Demokrasia uliangalia ukubwa wa matatizo yanayowakabili Watanzania wa kawaida pale wanapojihusisha na sekta ya sheria pamoja na urasimu. Katika sehemu inayofuata tunaangalia kile walichokibaini.

Kuelekea kwenye sheria ya watu

... wajasiriamali wengi wenye nia wanaendelea kubuni, wao wenyewe, mienendo, mbinu, na vyama kwa ajili ya kufanya biashara, kusajili na kulinda biashara na mali zao, kukuza biashara zao, kutumia ankara na mikataba yao, kufikia masoko mapya – yote haya ni kwa ajili ya kuongeza tija na kukua kiuchumi.

Wakiwa wamelazimika kuendesha shughuli zao katika mazingira ya mfumo wa sheria ambao huwabana, kuwabagua na kuwatenga, Watanzania, makumi kwa maelfu, walio katika sekta isiyotambulika kisheria, moja kwa moja hujikuta wakiunda sheria zao wenyewe – sheria ya watu.

[Ripoti ya Ubainishaji ya Taasisi ya Uhuru na Demokrasia Juz. 2 uk8]

⁷ Ripoti ya ubainishaji ya Taasisi ya Uhuru na Demokrasia inatoa mifano mingi kwa kina kuhusu mwelekeo huu mpya.

Sekta ya kisheria – gharama za muda na fedha



Mfumo wa kisheria kwa ajili ya kushughulikia mali na kuanzisha, kuendesha na kupanua na hatimaye kufunga biashara tayari upo nchini Tanzania. Hata hivyo, kwa mujibu wa utafiti wa Taasisi ya Uhuru na Demokrasia, ni asilimia 11 tu ya mali na asilimia 2 tu ya biashara zinazotumia mfumo huo. Kwa nini hali iko kama hivyo? Kimsingi, mfumo uliopo hauna uwazi, hautabiriki na hauna maana kiuchumi.

Masanduku mawili yafuatayo yanatoa mifano ya matatizo hayo na vikwazo vinavyowakwamisha watu masikini katika kujiunga na uchumi wa kisheria. Maelezo haya yanatokana na utafiti pamoja na mahojiano na watu wenyewe katika mazingira halisi ya Tanzania ya leo.⁸

Inagharimu nini kufanya biashara katika Sekta ya Kisheria Tanzania?

Kama Mjasiriamali wa Arusha ataamua kuanzisha biashara halali kisheria, njia rahisi ni kujisajili kama mmiliki halisi wa biashara hiyo. Hii itakuwa na maana kwamba atatumia saa 60 katika ofisi za serikali na itagharimu ada ya jumla ya dola 81 za Kimarekani. Baada ya kipindi cha wastani wa siku 86 ataweza kupata leseni ya kuendeshea biashara yake.

Baadae anaweza kuamua kuifanya biashara yake kama kampuni ya mtu binafsi ili kupunguza hatari za kuanguka kibiashara na/ au kukuza mtaji kutoka kwa washirika wengine. Zoezi hili litachukua saa nyingine 1,628 katika ofisi za serikali na kumgharimu kiasi cha dola 1,040 za Kimarekani.

Kama ana ndoto za kukuza biashara yake, itabidi atafute mkopo kutoka benki kwa kutumia mali aliyonayo kama amana ya mkopo. Hii itahitaji “uthibitisho wa kumiliki ardhi mijini, ”, idhini toka mipango miji, idhini ya kujenga pamoja na ada ya hati dhamana. Itagharimu kiasi cha dola 1,548 za Kimarekani na kuchukua saa 144 katika ofisi za Serikali kupata idhini – ambayo itapatikana baada ya siku 1,046.

Halafu kadri miaka itakavyopita kutakuwa na gharama nyingine za biashara. Saa 8 (dola 11 za Kimarekani) kulipia ada ya mwaka ya usajili wa biashara; saa 60 kila mara (dola 74 za Kimarekani) kupata kibali cha mwaka kwa ajili ya kujitangaza kihalali; saa 28 kila mara (dola 35 za Kimarekani) kupata bima ya kila mwaka; saa 96 kila mara (dola 993 za Kimarekani) kulipia ushuru; siku 164 (dola 2,539 za Kimarekani) kutatua migogoro na biashara nyingine na saa 48 (dola 1,783 za Kimarekani) “kufunga” kampuni yake.



⁸ Idadi iliyotumika ni wastani wa taifa. Maelezo yatatofautiana kati ya biashara moja na nyingine na kutoka eneo moja hadi lingine nchini kote.

Kwa kiasi gani sheria zilizopo zinagharimu biashara yako?

Kwa wastani, katika kipindi chote cha biashara itakayodumu kwa muda wa miaka 50 mjasiriamali atatakiwa kulipa dola 91,000 za Kimarekani na kutumia siku 1,118 (au miaka 4) katika ofisi za Serikali kutafuta leseni na vibali. (Katika kipindi hiki chote angekuwa amezalisha dola 9,350 za Kimarekani!) Kisha atatakiwa kusubiri siku nyingine 32,216 ili kupata vibali, huku akipoteza tena dola 79,600 za Kimarekani katika kipato chake.

Jumla kuu ya gharama hizi kubwa na zisizo za msingi ni karibu dola 180,000 za Kimarekani. Hiki ni kiasi kinachotosha kuanzisha biashara nyingine ndogondogo 31 katika Tanzania ya leo. Kama angekuwa ameiweka fedha hiyo benki kwa faida ya asilimia 5 kwa mwaka angekuwa amepata angalau dola 9,000 za Kimarekani kwa mwaka. Hii ni mara 33 ya Wastani wa Pato la Taifa kwa mwaka. Kama angeliingiza tena kiasi hicho cha dola 9,000 za Kimarekani kwenye kampuni yake angeweza kukuza biashara yake mara tatu kila mwaka.



Jedwali lifuatalo linaonyesha kifungu kidogo sana cha gharama na matatizo yanayohusiana na taratibu mbalimbali za kisheria. Utafiti na mahojiano yaliwarahisishia watafiti kugawa kila utaratibu kwenye hatua na ngazi kadhaa. Hizi zilitumika baadae kuhesabu idadi ya siku ambazo mtu wa kawaida angechukua katika kukamilisha taratibu zote na kiasi cha fedha ambazo angetumia. Matokeo haya yanashitua na kuwa na maelezo marefu ya kufafanua kwa nini watu wengi masikini walazimishwe kufanya shughuli zao kwenye sekta isiyo rasmi.

Jedwali la 4: Mifano ya gharama za kufuatilia taratibu za kisheria

Utaratibu:	Hatua	Ngazi	Siku	Gharama
Kuanzisha kampuni binafsi kisheria (Ofisi ya Kubadili Fedha) Mbeya	10	103	379	US\$5,506
Kutatua migogoro ya kibiashara mahakamani (madai ya madeni)	9	96	390	US\$ 11,964
Kukusanya madeni kwa kutumia agizo la mahakama	5	7	1286	US\$1,022
Kugawa ardhi kwa ajili ya ujenzi na kupata kibali cha kujenga	13	68	2920	US\$2,252

Je, mabadiliko gani ni ya lazima?



Ili kuwarahisishia Watanzania wengi au hata wote kutumia mfumo rasmi itabidi kufanya mabadiliko yatakayooanisha pamoja, mfumo rasmi na ule usio rasmi na kuunda mfumo mmoja utakaowanufaisha watu wote.

Mfumo rasmi na halali kisheria uliopo hauna budi kurahisishwa na kurekebisha ili uwiane na mahitaji ya Watanzania wengi ambao wanatumia sekta isiyo rasmi⁹. Aidha, taratibu na nyaraka mbalimbali za sekta isiyo rasmi hazina budi kurekebisha ili ziwe rasmi zaidi na zioane na mfumo rasmi ulioboreshwa. Hii itahusisha mabadiliko ya kimuundo kutoka juu kwenda chini na pia kutoka chini kwenda juu.

Mara mabadiliko haya yatakapokuwa yamefanyika kutakuwa na sheria ya aina moja badala ya sheria mbili na uchumi utapanuka kiasi cha kuweza kuwahusisha watu wote katika jamii. Msingi wa marekebisho unajibainisha hatua kwa hatua kadri majadiliano na wadau yanavyoendelea.

Endapo mfumo rahisi na unaotekelezeka wa kisheria na kirasimu utanzishwa, bila shaka utawarahisishia Watanzania kushiriki zaidi katika uchumi. Kwa mfano, kama watanzania wanaweza kusajili biashara zao katika ngazi moja au mbili kwa kutembelea ofisi iliyo jirani na mahali wanapoishi, kwa vyovyote vile wangependelea zaidi kufanya hivyo. Kama usajili wa biashara umefanyika kwa kutumia fomu ya utambulisho inayokubalika kisheria ambayo itaondoa wasiwasi kwa wateja na wagavi wa bidhaa wa kushirikiana na mwenye biashara, kwa vyovyote vile biashara hiyo inaweza kupanuka na kuenea katika eneo kubwa zaidi. Kufanya hivi kutaboresha mfumo wa jadi wa kumwomba Afisa Mtendaji wa Kijiji au Mwenyekiti wa Kijiji kuweka saina kwenye fomu isiyo rasmi ya kitambulisho, ambayo kwa kiasi kikubwa inaweza isikubalike.

Vivyo hivyo, kama urasimishaji una maana ya kuonyesha kwamba inawezekana kupata hati ya kumiliki ardhi katika hatua chache, badala ya kujaza fomu nyingi na kutumia siku nyingi za kwenda kwenye ofisi mbalimbali, itawarahisishia watu wengi kuandikisha na kusajili ardhi na mali zao.

Hata hivyo, kama urasimishaji ni kwa ajili ya kuwawezesha Watanzania wengi wanufaike na nafasi zinazotolewa na mfumo mmoja wa kitaifa wa haki mali na uanzishaji wa biashara, patahitajika mambo mengine zaidi. Mambo hayo yataandaliwa kwa kutumia msingi wa nyenzo za kiuchumi utakaoandaliwa na MKURABITA na yatatatua matatizo mbalimbali yanayowakabili Watanzania wanaotaka kuongeza ushiriki katika uchumi wao.

MAMBO MUHIMU – MASUALA MENGINE YA MKURABITA



1. Watu wanahitaji mafunzo ili wafanikiwe kwenye uchumi rasmi

Watu wanaofanya kazi katika sekta isiyo rasmi, kwa maneno mengine, idadi kubwa ya Watanzania, itabidi wapatiwe stadi za msingi za upanuzi wa biashara zao katika sekta rasmi. Kwa sasa watu wengi katika sekta isiyo rasmi wana kiwango kidogo cha maarifa ya biashara, taarifa chache za masoko na teknolojia duni ya uzalishaji. Vilevile, vyama vya biashara katika sekta isiyo rasmi vinalegalega kiupangaji na kiusimamizi. Kwa walio wengi katika sekta isiyo

⁹ Tazama maelezo ya 3 kwa ajili ya mifano. Hizi zinahusiana na mabadiliko ya sekta ya umma pamoja na uboreshaji wa Haki Mali, Fomu za kuendesha biashara na upanuzi wa masoko.

rasmi, kuboreshwa kwa haki mali na usajili wa biashara peke yake havitoshi kuwafanya wafanikiwe: wote katika sekta isiyo rasmi watahitaji mafunzo, taarifa na uimarishaji wa vyama vyao.

Hata hivyo, kwa sasa hivi idara nyingi za serikali na mamlaka za mitaa hazijaboreshwa ili kuweza kutoa mafunzo ya kibiashara kwa watu wengi kutokana na sababu mbalimbali, ikiwemo ukosefu wa watumishi wa ugani.

2. Taasisi za fedha lazima ziwe na nia ya kukopesha miradi midogomidogo na ya kati

Kwa sasa, watu masikini na wenye biashara ndogondogo wanapata shida sana kupata mikopo kwenye taasisi za fedha. Sababu mojawapo ni kwamba benki ni lazima zifanye kazi kwa mujibu wa sheria, zilizowekwa na Benki Kuu ya Tanzania, ili kuepuka matatizo yanayoweza kujitokeza katika kuwahudumia wateja wao. Ni muhimu sana kupitia sheria hizi ili kuziwezesha benki hizi kuwasaidia watu kuzitumia rasilimali zao zilizorasimishwa. Hii ni moja kati ya kazi nyingi zitakazohitaji kufanyika ili kuongeza utoaji wa mikopo kwa wakopaji wadogo.

3. Unahitajika mfumo unaokubalika wa utambulisho wa mtu binafsi

Kama mali au biashara imesajiliwa kwa kutumia jina la mtu, tungependa kuwa na uhakika kama kweli mtu huyo ni yule aliyesimama mbele yetu! Ili kufanikisha hili unahitajika mfumo wa vitambulisho vya uraia ili kutuwezesha kukagua biashara za kitaifa na mitaa pamoja na rejesta za mali na kufahamu kama mtu huyu anakopesheka au anafaa kuwa mshirika kibiashara.

4. Utunzaji wa kumbukumbu za serikali za mitaa lazima uboreshwe

Kwa sasa, serikali nyingi za mitaa zinatumia mfumo wa kuandika kumbukumbu kwa mkono. Mara nyingi, ujazaji mbaya na ucheleweshaji unaotokana na urasimu vinaweza kuwa kikwazo kwa watu wanaojaribu kujisajili na kupata kumbukumbu. Ni muhimu kuziweka kumbukumbu zote za ardhi na biashara kwenye kompyuta ili kuwapunguzia gharama za ucheleweshaji watu walio na muda na fedha chache.

5. Utawala na upatikanaji wa haki lazima uboreshwe

Kama watu masikini watahamasishwa kurasimisha mali zao ni lazima wapate uhakika kwamba serikali na mahakama zitawatendea haki. Wawe na uhakika kuwa utawala hautawakejeli na kwamba matajiri hawatapewa upendeleo. Utekelezaji na uimarishaji wa viwango lazima utiliwe maanani. Mfumo wa kodi uwe wa haki na mfumo wa mahakama uweze kufikiwa na kila mtu.

Sehemu ya 3 itajadili mapendekezo yanayopendekezwa kwa upana kidogo.



3. Marekebisho ya MKURABITA - Nini kinapendekezwa?

Hapa tutaangalia baadhi ya marekebisho ambayo yamejadiliwa katika hatua ya sasa ya Muundo wa Marekebisho ya MKURABITA. Ili kushughulikia masuala haya, itabidi Serikali pamoja na Bunge waamue aina ya marekebisho yanayohitajika katika sheria, taratibu na mipango ya serikali. Baadhi ya mapendekezo muhimu yaliyopendekezwa hapa yanaweza kupitishwa, mengine yanaweza yakaachwa; mengine yanaweza kutekelezwa haraka, na mengine yakachukua muda mrefu. Kwa kuangalia mapendekezo haya unaweza kuanza kuona ni kwa jinsi gani MKURABITA inakufaa.

Kama tulivyoona mwanzoni mwa mwongozo huu, malengo ya MKURABITA ni kuwawezesha watu wengi waliokosa fursa kwa kuwa kwenye sekta isiyo rasmi watumie mali na biashara zao na kufaidika na manufaa mengine katika uchumi wa soko wa kisasa. Marekebisho haya yanakusudiwa kuviwezesha vikundi lengwa¹⁰ kupanua biashara zao, kuongeza kipato na kushiriki katika upunguzaji wa umasikini.

Hivyo, ni mapendekezo ya namna gani ya kuutekeleza mkakati huu na kufikia malengo ya programu ya MKURABITA? Tutajadili masuala yaliyopendekezwa kufanyiwa marekebisho na shughuli zinazohusiana nayo katika vichwa vya habari vinne:

1. Rahisisha upatikanaji wa haki bayana za kumiliki ardhi na uhamishaji wake
2. Rahisisha uendeshaji wa biashara kihalali na kwa faida
3. Rahisisha upatikanaji wa mikopo pamoja na huduma nyingine za fedha
4. Anzisha mfumo madhubuti wa taarifa

Kwa kiasi kikubwa, utekelezaji wa marekebisho utatofautiana Tanzania Bara na Visiwani, kutokana na tofauti za sheria na mifumo ya utawala katika sehemu hizi mbili za Jamuhuri ya Muungano. Hata hivyo, masuala ya msingi katika mapendekezo mengi ya marekebisho yanahusu pande zote mbili. Pitia marekebisho yanayopendekezwa kisha jaribu kubaini yale yanayokuhusu moja kwa moja.

1. Rahisisha upatikanaji wa haki bayana za kumiliki ardhi na uhamishaji wake

Watumiaji wengi wa ardhi vijijini wana haki ya kumiliki na kutumia ardhi wanayokalia sasa (Haki ya Kimila ya Kumiliki) lakini hawana hati rasmi ya umiliki. Katika miji, mipango miji hairekebishwi mara kwa mara ili kuwiana na ongezeko la watu na maendeleo na haitengi maeneo ya kutosha ya biashara mpya pasipo wamiliki kuhofia kufukuzwa. Watu wengi wanaoishi katika maeneo ya miji yasiyopimwa hawana hata haki kisheria ya kumiliki viwanja vyao (ingawa kwa Dar es Salaam hivi karibuni baadhi ya watu wamepatiwa hati za muda zinazowahakikishia usalama kwa kiasi fulani). Kama unataka hati ya kumiliki kiwanja chako, mchakato wa kukipima na kuomba hati hiyo ni wa taratibu sana na ghali, hasa vijijini.

Kuwa na hati ya kumiliki ardhi yako kunaweza kukusaidia kudhibiti eneo lako. Hata hivyo, pamoja na hati hiyo, bado inaweza kuwa vigumu kukwepa migogoro inayohusiana na ardhi yako. Hii inatokana na ukweli kwamba hakuna mfumo rasmi unaoeleweka wa kuandikisha hati hizo na nyaraka nyingine zinazokupa haki ya kutumia ardhi (kama vile kumkodisha jirani yako sehemu ya ardhi yako, au kile mnachokubaliana mnapotatua mgogoro wa mpaka na jirani yako). Kwa sababu hiyo, maafisa tofauti huweza kutoa hati ya kumili kiwanja kimoja kwa watu tofauti. Wakopeshaji kama vile benki wanaotaka kutumia ardhi kama dhamana ya mkopo hawawezi kupata taarifa za uhakika za hati yako na haki zozote (kama vile ukodishaji) ambazo umewapatia watu wengine. Kunapokosekana usajili wa kuaminika wa haki za ardhi, ni vigumu sana kujua kama haki za wanandoa na watoto zinalindwa.

Marekebisho gani yanazingatiwa?

- **Anzisha taratibu rahisi na zinazokubalika kwa ajili ya kutunza na kusajili mikataba na makubaliano yanayohusu ardhi**

→ Harakisha uanzishaji wa rejesta za vijiji (mijini hizi huitwa rejesta za serikali za mitaa), na wape viongozi wa serikali za mitaa mamlaka ya kupitisha na kusajili nyaraka zinazohusiana na ardhi.

***Tanbihi:** tazama Eneo la Marekebisho la 4 kwa ajili ya kupata maelezo zaidi kuhusu namna ambavyo mfumo wa usajili wa nyaraka za ardhi ungeweza kuboreshwa zaidi.*

- **Anzisha taratibu rahisi na zinazokubalika kwa ajili ya kutatua migogoro ya ardhi**

→ Toa mafunzo kwa viongozi wa mitaa, mf. Maafisa Watendaji wa Kijiji au Mtaa, kuwasaidia watu wenye migogoro ya ardhi waweze kufikia makubaliano bayana yanayotekelezeka kisheria. Toa miongozo ya upatanisho kwa ajili ya viongozi hawa na Baraza la Ardhi la Kijiji na Mabaraza ya Kata. Hii ihusishe pia utumiaji wa fomu mpya zinazokubalika katika kuweka kumbukumbu muhimu kuhusu makubaliano hayo, kuidhinisha fomu hizo na kutunza nakala kwenye mfumo mzuri wa majalada ili watu wanaohusika na ardhi hiyo waweze kuona kilichokubaliwa.

→ Badala ya kuteuliwa na Waziri wa Ardhi, mamlaka za mitaa zingeweza kuteua wapatanishi wa migogoro ya mipaka ya ardhi ya kijiji. Mipango ya matumizi na umilikishaji wa ardhi inaweza kuendelea katika maeneo ambayo hayana migogoro.

- **Rahisisha upatikanaji wa hati miliki rasmi ya ardhi**

→ Harakisha mchakato wa upimaji wa ardhi ya kijiji na utoaji wa hati ya kumiliki. Ramani ya mipaka ya kijiji pamoja na hati ya umiliki wa ardhi yote ya kijiji ingeweza kuidhinishwa wilayani, badala ya Wizarani. Badala ya kutegemea maafisa wa wilaya, maafisa wa kata na vijiji wangeweza kupatiwa mafunzo ili kusaidia mipango ya matumizi shirikishi ya ardhi kwa wanakijiji.

→ Ili kuokoa muda na fedha, vijiji vipewe 'hati miliki za mkupuo' kwa kila eneo linalomilikiwa na mwanakijiji mmojammoja. Maafisa Watendaji wa Vijiji na

maafisa kata wangeweza kupewa vifaa vya upimaji vinavyobebeka pamoja na mafunzo ya namna ya kuvitumia yatakayowasaidia katika utekelezaji wa jukumu hili. Badala ya kutumia fomu tatu, fomu moja tu ingeweza kutumika kuombea hati ya kumiliki eneo, na watu wenye haki ya kimila ya kumiliki ardhi wangeweza kupatiwa hati pasipo kuombwa barua ya kuthibitisha.

- Ardhi ya jumuiya Vijijini na maeneo ya umma mjini yangewekewa mipaka na kulindwa.
- Harakisha mchakato wa “kuhalalisha” makazi yasiyo rasmi ya mjini. Hii ingehusisha kutumia wataalamu binafsi wa mipango miji, badala ya hali ya sasa ya kusubiri maamuzi yafanywe na Wizara ya Ardhi, katika kuandaa mipango ya kuhalalisha makazi na kupima upya viwanja pasipo kusubiri ujenzi wa miundombinu na huduma muhimu. Uboreshaji wa usajili wa hati miliki kimtaa ungeweza pia kusaidia (tazama Eneo la Marekebisho la 4).
- Boresha michakato ya mipango miji. Mipango miji ingeweza kuingiza taratibu za kuhakikisha kuwa maeneo ya kutosha vinatengwa kwa ajili ya wafanya biashara wadogowadogo.

- **Rahisisha uhamishaji wa haki na hati miliki (zikiwamo Haki za Kimila za Umiliki Ardhi)**

- Harakisha taratibu za kuuza au kuhamisha umiliki wa ardhi: wezesha umiliki wa ardhi uweze kuhamishwa pasipo kusubiri viongozi wachunguze kama ardhi imetumika vizuri na kulipiwa kodi, rahisisha utaratibu wa ulipaji wa kodi ya ardhi; badala ya Afisa wa Ardhi, msajili au mnunuzi anaweza kuthibitisha kwamba waraka wa mauzo upo sahihi kisheria.
- Fanya nyaraka za usajili wa ardhi ziwe sahihi na kamilifu vya kutosha ili watu wanaonunua na kuuza ardhi wawe na uhakika kwamba hakuna matatizo au madai yaliyojificha.

2. Rahisisha uendeshaji wa biashara kisheria na kwa faida

Kwa sasa, taratibu ngumu na zisizo na manufaa zinawakatisha tamaa wafanya biashara ndogongogo kuingia kwenye biashara rasmi. Kusajili biashara na kupata leseni hugarimu fedha na muda mwingi, na masharti ya leseni hayaeleweki na hayabadiliki. Hakuna fomu rahisi ya usajili wa biashara kwa watu wengi walio katika sekta zisizo rasmi ambao hufanya biashara zao kama kikundi au chama.

Inaweza kuwa ngumu sana kutekeleza mkataba wa kibiashara. Watu wengi hawana uwezo wa kutumia mahakama katika kutatua migogoro ya kibiashara, hata hivyo mbinu rahisi na za haraka haraka kama vile usuluhishi zinaweza zisiwe za kufaa kwa sababu hazifanywi kwa kufuata taratibu za kueleweka. Aidha endapo shauri litapelekwa mahakamani, ni mikataba iliyo na sifa fulani tu na iliyoidhinishwa na kusajiliwa ndiyo inayoweza kuthibitisha bila utata wa kile kilichoamuliwa.

Hata kama wamesajiliwa na kuwa na leseni, waendeshaji wengi wadogowadogo katika sekta isiyo rasmi bado wanahitaji maeneo mazuri ambako watafanya biashara zao bila hofu ya kufukuzwa (tazama Eneo la Marekebisho la 1, hapo juu). Pia wanahitaji taarifa, ushauri na mafunzo kwa ajili ya kuboresha biashara zao hadi kufikia kiwango cha kuwawezesha kunufaika kutokana na mazingira ya biashara rasmi zaidi: kwa mfano, kutunza mahesabu ya biashara katika kiwango kinachokubalika kwa wenye mablenki na kwa mamlaka ya mapato. Aina hii ya msaada utapatikana kirahisi zaidi kupitia vyama makini vya biashara.



Marekebisho gani yanazingatiwa?

- **Rahisisha usajili na upatikanaji wa leseni ya biashara**

- Taratibu za kusajili biashara zirahisishwe kwa kiwango kikubwa ili kupunguza upotevu wa fedha na muda. Suala hili litatuliwe kupitia programu ya MKUMBITA.
- Matatizo binafsi ya kuyumba kifedha kwa baadhi ya wafanya biashara yapunguzwe kwa kuanzisha shirika za 'deni ukomo' kwa wafanyabiashara walioko katika kikundi, pamoja na 'deni ukomo' kwa wamiliki binafsi kwa wanaoendesha biashara binafsi. 'Deni ukomo' hutenganisha kabisa fedha na mali za biashara na zile za mmiliki, hivyo mmiliki halazimiki kulipa madeni yote ya biashara endapo biashara husika itaanguka.

- **Weka taratibu rahisi na zinazokubalika kwa ajili ya kutunza na kusajili mikataba ya biashara yenye nguvu kisheria.**

→ Fomu rahisi na zinazokubalika kisheria kwa ajili ya mikataba ya kawaida ya biashara zitolewe kupitia Maafisa Watendaji wa Vijiji na Mitaa. Fomu hizi ni pamoja na zile za manunuzi, mikopo, kupangisha na za aina nyingine ya mikataba ya kawaida . Fomu ziwe na sifa muhimu za kisheria zinazohusu mikataba. Maafisa watendaji wa Vijiji na Mitaa wapewe mwongozo na mafunzo kuhusu uidhinishaji na usajili wa mikataba, na gharama za kazi hiyo zitokane na kodi ya huduma.

- **Rahisisha utumiaji wa huduma za usuluhishi na Upatanishi za maeneo husika katika kutatua migogoro ya kibiashara, badala ya kutumia mahakama ambazo gharama zake ni kubwa na huchukua muda mrefu.**

→ Viongozi wa maeneo husika mf. Maafisa Watendaji wa Vijiji au Mitaa wapatiwe mafunzo ya kuwasaidia watu katika kutatua migogoro ya ardhi na kufikia usuluhishi wenye nguvu kisheria. Patolewe miongozo ya usuluhishi kwa viongozi hawa na kwa Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na Kata. Hili litajumuisha pamoja na kutumia fomu mpya zinazokubalika kisheria katika kuandika mambo ya msingi katika makubaliano husika na kuidhinisha fomu na kutunza nakala katika utaratibu mzuri wa mafaili ili watu wanaohusika na ardhi hiyo wayaone makubaliano hayo.

→ Huduma rasmi ya kusuluhisha na kupatanisha pia ianzishwe (itumie wapatanishi waliopatiwa mafunzo, siyo wanasheria) ili kusaidia kutatua matatizo ya kibiashara kwa haraka na kwa urahisi pasipo kwenda mahakamani.

→ Sheria ibadilishwe ili kuziwezesha mahakama za mwanzo kuidhinisha makubaliano yaliyofikiwa kwa kutumia mchakato unaokubalika wa upatanishi au usuluhishi, na mahakama zinyang'anywe uwezo wa kubadili makubaliano yaliyofikiwa.

- **Wezesha wafanyabiashara wa sekta isiyo rasmi kupata maarifa na ujuzi unaohitajika katika kufanikisha biashara katika uchumi rasmi.**

→ Miongozo rahisi itolewe kwa wafanyabiashara ndogondogo ikiwaonyesha namna ambavyo wangeweza kuzingatia sheria: kwa mfano, namna ya kuandaa vizuri hesabu za fedha, kulipa kiasi kinachostahili cha kodi na kuzingatia sheria za kazi. Mafunzo katika maeneo haya na mengine ya usimamizi wa biashara yafikishwe hadi kwenye biashara ndogondogo nyingi zaidi. Taratibu nzuri ziandaliwe kwa ajili ya kuwapatia wafanya biashara ndogondogo taarifa kuhusu huduma za fedha pamoja na huduma nyingine zinazopatikana.

→ Huduma za namna hii zitolewe na asasi zilizopo kama vile Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogovidogo, ofisi ya msajili wa biashara (tazama Eneo la Marekebisho la 4, hapa chini), au na vitengo vingine vilivyoanzishwa kwa lengo la kufanikisha uingizaji wa biashara ndogongogo katika uchumi rasmi.

→ Jenga uwezo wa vyama vya biashara ili viwahudumie wanachama wao vizuri.

- **Weka kanuni kwa ajili ya kurahisisha taratibu za kiutawala**

→ Sheria mpya ya Jumla ya Kanuni za Utawala ianzishwe kuhakikisha kwamba kila idara ya serikali ina aina moja ya kanuni, na taratibu hizo zinakuwa wazi na rahisi

kadri inavyowezekana kwa watu maskini kuzielewa. Sheria ibainishe viwango kwa ajili ya viongozi kutekeleza majukumu yao kisheria, kiwajibu na kwa haki, ili kuondokana na upotezaji wa muda na kwa ajili ya kushughulikia mirejesho na malalamiko ya umma.

Kodi zinazolipwa na biashara ndogondogo zirahisishwe, ziwe zinazokadirika na zinazolipika.



3. Rahisisha upatikanaji wa mikopo na huduma nyingine za fedha

Inaweza kuwa ngumu sana kwa watu kupata mikopo kwa ajili ya kuanzisha, kudumisha au kupanua biashara zao (bila kujali kama shughuli yenyewe inahusu shamba dogo au karakana). Njia mojawapo ya kuhamasisha ukopaji ni kurahisisha utumiaji wa ardhi au mali nyingine kama dhamana ya kuchukulia mkopo – au kwa maana nyingine kupunguza kiwango cha hofu kwa mkopeshaji. Kwa sasa hakuna mfumo halali wa kusajili dhamana (ambapo mali inayohamishika kama vile redio au gari au mavuno yanayotarajiwa hutumika kama dhamana ya mkopo). Hivyo basi, benki inayotoa mikopo kwa ajili ya kilimo haiwezi kuwa na uhakika kama dhamana ya mkopaji - baadhi ya mavuno yanayotarajiwa, au baiskeli- tayari ilishatumika kama dhamana ya mkopo kwa mkopeshaji mwingine. Vivyo hivyo, rehani (ambapo mali ardhi imetumika kama dhamana ya mkopo) mara nyingi haisajiliwi kikamilifu kiasi kwamba huwa vigumu kwa benki kubaini kama tayari mali hiyo imeshawekwa dhamana kwenye benki nyingine au la.

Marekebisho gani yanazingatiwa?

- **Rahisisha utumiaji wa ardhi na rasilimali nyingine kama dhamana ya mkopo.**

→Utaratibu uanzishwe kwa ajili ya kusajili dhamana katika kijiji au ofisi ya msajili wa mtaa. Dhamana ya mavuno isajiliwe kwenye Ofisi ya Msajili Ardhi wa Kijiji.

→Mchakato wa kuandaa dhamana au rehani urahisishwe kwa kutumia fomu rahisi zinazokubalika kisheria, kuondoa baadhi ya ukaguzi wa awali, kurahisisha utoaji wa kodi katika masuala ya malipo ya ardhi na kuwezesha mthibitishaji au msajili kuidhinisha uhalali wa kisheria wa rehani (badala ya kutumia Afisa Ardhi wa Wilaya).

- **Rahisisha upatikanaji na usalama wa mikopo toka benki**

→Kuwa na hati ya kumiliki ardhi au nyumba kunaweza kumsaidia mkopaji kupata mkopo – ama kwa kuitumia kama dhamana ya mkopo au kama njia mojawapo ya kitambulisho na anuani zao.

→Watu wataweza kupata mikopo kwa urahisi zaidi kama wakiwa na fomu za utambulisho zinazokubalika kisheria. (tazama Eneo la Marekebisho la 4 hapa chini).

→Fomu ya usajili lazima iwe na taarifa zinazoeleweka kuhusu mwenzi au wenzi wanaomiliki ardhi.

→Asasi za kifedha zinazokubali ardhi kama dhamana ya mkopo kwa kutumia taarifa zilizotolewa na Ofisi ya Msajili Ardhi wa Kijiji au Mtaa zilindwe dhidi ya kupoteza dhamana husika: hivyo mtu aliyekuwa na haki ya kumiliki ardhi ambayo haijasajiliwa asiweze kuzuia ardhi yake kuchukuliwa endapo mkopo aliokopa haukulipwa.

→Serikali ishirikiane na Chama cha Wenye Mabenki Tanzania katika kuyapitia masharti ya ukopeshaji wafanyabiashara ndogondogo na kuweka utaratibu wa dhamana kwa mikopo ya biashara ndogongogo. Kanuni za Benki Kuu ya Tanzania za tahadhari zinazopaswa kuchukuliwa na mabenki wakati wa kutoa mikopo midogomidogo zilegezwe ili iwe rahisi kwa mabenki kutoa mikopo.

→Endapo mkopo uliochukuliwa hautalipwa, mkopeshaji atumie mtaalamu wa huduma ya upatanishi na usuluhishi (tazama hapa chini) ili kuchukua mali ya mkopaji (ardhi au mali nyingine) badala ya kwenda mahakamani.

→Taasisi ya Kumbukumbu za Mikopo ianzishwe ili kuzisaidia benki katika kutathmini waombaji wa mikopo (tazama Eneo la Marekebisho la 4, chini).

4. Weka mfumo bora wa mawasiliano

Mfumo bora wa kuratibu habari unaweza kusaidia katika kujibu maswali muhimu. Je mtu au kampuni hii inaaminika kufanya nayo biashara au kuikopesha fedha? Je kuna mgogoro wa mpaka katika ardhi hii ninayotaka kuikodisha? Je mtu mwingine

ana hatimiliki ya ardhi hii? Kama mwenza katika ndoa je haki zangu kwa ardhi zimesajiliwa? Je mkopaji huyu tayari ameshaweka cherehani yake kama dhamana kwenye asasi nyingine ya mikopo midogomidogo? Kama meneja wa benki, je ninaweza kuikubali ardhi hii kama dhamana kwa mkopo wa kujenga nyumba, au tayari imeshachukuliwa na mkopaji mwingine?

Ni vigumu kupata taarifa za kuaminika kuhusu mtu au kampuni ili kuona kama yale wanayosema kuwahusu ni sahihi. Hakuna waraka unaokubalika kisheria ambao mtu anaweza kuutumia katika kuthibitisha utambulisho wa mhusika. Mtu au kampuni inaweza kuwa na madeni kwa wakopaji wengi, lakini hakuna mahali unapoweza kupata taarifa hizo. Hali hii hujenga hofu ya kupata hasara ikiwe utafanya biashara na watu au kampuni binafsi usizozijua– na mara nyingine hata kwa watu unaowajua. Taarifa kuhusu ardhi zinaweza kutunzwa sehemu mbalimbali na kwenye fomu tofauti.

Taarifa za umma hutunzwa masjala (kuanzia ngazi ya vijiji hadi taifa), lakini nyaraka hazijaandaliwa ipasavyo kisheria, na mafaili hayahifadhiwi kwa njia ya kuhakikisha usalama wa nyaraka na kuziwezesha kupatikana kwa haraka pindi zinapohitajika. Kuna ofisi tofauti tofauti za masjala kwa ajili ya shughuli mbalimbali, hali ambayo husababisha gharama za ziada na kupunguza ufanisi.

Marekebicho gani yanazingatiwa?

- **Anzisha mtandao ulio wazi na unaopatikana wa masjala za kutunzia kumbukumbu za mikataba na makubaliano.**

→ Anzisha masjala moja katika ngazi ya kijiji au mtaa kwa ajili ya kutunzia mikataba na makubaliano yote yanayohusu ardhi, biashara, migogoro na masuala mengine. Maofisa Watendaji wa Vijiji na Kata wapewe mafunzo na kupatiwa muundo na kanuni zinazokubalika kisheria katika kuandika makubaliano na mikataba, na katika kuidhinisha, kusajili na kuzijaza kwa usahihi. Huduma hii ilipiwe kwa ada rasmi kwa kila waraka.

→ Makubaliano yaliyofanywa awali yanaweza kusajiliwa kama taarifa muhimu kuhusu makubaliano hayo zitanakiliwa kwenye fomu zilizokubalika kisheria.

→ Watendaji wa Vijiji na Viongozi Watendaji wa Kata watume nakala ya kila waraka uliosajiliwa kwenda Masjala ya Wilaya, ambayo itaifungulia faili na kutuma taarifa za msingi kuhusu waraka husika kwenye Masjala ya Kanda (kuna kanda sita nchini Tanzania).

Je ulijua?

Waraka uliosajiliwa katika masjala ya wazi unakubalika kama uthibitisho wa kisheria wa makubaliano ya pande mbili. Kila mtu ana haki ya kisheria kuona waraka wowote uliosajiliwa wazi (lakini atatakiwa kulipa ada rasmi kwa huduma hii).

- **Weka mfumo mmoja wa usajili wa ardhi**

→ Ofisi tatu kuu za usajili wa umiliki wa ardhi (Ofisi ya Kijiji ya Usajili wa Ardhi, Ofisi ya Mtaa ya Usajili wa Ardhi na Ofisi ya Usajili wa Hatimiliki ya Kijiji/Mtaa) zinaweza kufanya kazi kwa njia ya ushirikiano zaidi, kwa kutumia viwango vinavyofanana vya uandikaji nyaraka, usajili na uingizaji katika

mafaili, na kupeleka taarifa kwenye kituo kikuu ambacho kitahakikisha mfumo mzima unatoa taarifa za kuaminika.

- **Anzisha mfumo shirikishi na rahisi wa masjala ya biashara na habari za biashara.**

→ Viwango vya msingi vya uhifadhi nyaraka, usajili na ujazaji fomu vitumike katika ofisi zote za usajili wa biashara na vyama vya biashara.

→ Kwa hali hiyo, masjala tofauti (kwa ajili ya makampuni, majina ya biashara na vyama vya ushirika) yaunganishwe kuunda ofisi moja ya usajili kwa kutumia namba tofauti kwa kila biashara ambayo itatumika kama utambulisho katika shughuli zote. Ofisi hii ya usajili ipewe jukumu la kuhakikisha kuwa leseni zote za biashara zinatolewa au zinakataliwa ndani ya muda maalum. Pia itoe taarifa za kawaida kwa makampuni yote yaliyosajiliwa zitakazoyasaidia katika kuzingatia sheria.

→ Taasisi ya Kumbukumbu za Mikopo ianzishwe kwa lengo la kutoa taarifa kwa wakopeshaji au washirika wa biashara kuhusu jinsi ambavyo watu au biashara zimetimiza majukumu yao ya kifedha. Taarifa hii iingizwe moja kwa moja kutoka vyanzo mbalimbali: ofisi za usajili wa ardhi na biashara, mamlaka ya mapato, TANESCO na asasi nyingine zinazouza kwa mkopo. Taarifa hii inaweza kuunganishwa pia na Benki Mpya ya Data za Kumbukumbu za Mikopo iliyoanzishwa mwaka 2006 ili kutoa taarifa kuhusu wakopaji ambao wamekiuka kulipa madeni yao benki. Watu lazima wapate uwezo wa kuona taarifa iliyowekwa kuwahuu wao, na kutakuwa na kanuni zilizo wazi kuhusu nani anaweza kuomba taarifa.

- **Weka mfumo maalumu wa utambulisho.**

→ Serikali inapanga kutoa vitambulisho vya kitaifa ambavyo vitakuwa na namba ya kipekee kwa kila mtu. Pamoja na hivyo, barua kutoka kwa wenyeviti wa Vijiji au Mitaa ambazo huthibitisha anwani za wakazi au sifa zao binafsi zigeuzwe kuwa hati rasmi za ukazi au sifa binafsi, katika muundo maalumu. Barua hizi zithibitishwe na afisa mtendaji wa kijiji/mtaa na kurekodiwa kwenye kitabu cha usajili cha wakazi – na zisainiwe Wilayani pale ambapo itabidi zitumike kwingineko nchini.



Kumbuka:
Marekebisho haya ni mapendekezo tu katika hatua hii. Yanajadiliwa na vikundi mbalimbali vya wadau. Katika Sehemu ya 2 ya kitabu hiki tutaangalia baadhi ya maswali yanayoulizwa kuhusu MKURABITA. Kupitia maswali haya na majibu yao tunaangalia baadhi ya mitazamo na matatizo ya wadau ambao tayari wametoa maoni kuhusu mpango huu.

4. MKURABITA - Majukumu na mahusiano

Katika sehemu hii tunatazama wahusika katika utekelezaji wa MKURABITA na tunatazama pia baadhi ya programu za Serikali zinazochangia katika marekebisho ya MKURABITA.

MKURABITA – nani anawajibika?

MKURABITA ni programu endelevu itakayohusisha watu wengi zaidi kadri muda unavyopita. Katika hatua za awali kuna vikundi vitatu vya washiriki ambavyo majukumu yao ni kama yafuatavyo:

Serikali ya Tanzania

- Inatoa uongozi wa kisiasa
- Inaendeleza uwajibikaji na kuifanya Programu kuwa ajenda ya kipaumbele
- Inatoa maamuzi muhimu na ya kimkakati

Kitengo cha Uendeshaji wa Programu (PMU)

- Kinatoa msaada wa kitaalamu, kiutawala na kiutaratibu
- Kinasaidia ushirikiano wa ofisi za serikali na wadau
- Kinafanya kampeni za uhamasishaji na mawasiliano

Taasisi ya Uhuru na Demokrasia (ILD)

- Inatoa uongozi wa kitaalamu
- Inafafanua masuala muhimu
- Inafanya utafiti
- Inaandaa mapendekezo na mipango ya mageuzi

Mageuzi haya yanaweza kutekelezwa na programu zilizopo za serikali, au zinahitajika asasi mpya za 'MKURABITA'?



Programu nyingi za serikali zilizopo zinashughulikia baadhi ya maeneo ya marekebisho yanayozingatiwa katika MKURABITA. Hivi ni baadhi ya vipengele vya programu tatu zinazohusika zaidi.

Mpango ya Kuimarisha Mazingira ya Biashara Tanzania(MKUMBITA) inayoratibiwa na Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezesaji imekusudiwa kushughulikia masuala kadhaa muhimu kama ya MKURABITA. Madhumuni yake ni kuwarahisishia watanzania na wageni kuendesha biashara kwa faida. Inafadhiliwa na wafadhili mbalimbali wa nje ya nchi na Benki ya dunia. MKUMBITA imetoa fedha kwa 'Kitengo cha Kanuni Bora' kilichopo wizarani ambacho kinahusika na kutoa ushauri wa mabadiliko ya sheria na kanuni ili kuondoa vikwazo visivyo na msingi katika biashara. Kitengo hiki kimeanzisha sheria mpya – Sheria ya Usajili wa Shughuli za Biashara - ya kusajili na kukata leseni za biashara kirahisi na kiufanisi zaidi.

Mpango wa kimkakati wa kutekeleza sheria za ardhi (SPILL) unaoendeshwa na Wizara ya Ardhi, umekuwa ukijaribu kupima na kutoa hatimiliki kwa ardhi ya vijijini na mijini, na kuanzisha masijala za kuhifadha nyaraka za ardhi. Hii ni pamoja na utoaji wa leseni rasmi kwa watu za kuendelea kuishi kwenye makazi yao yanayopimwa jijini Dar es Salaam. Hati hizi ni za muda wa miaka miwili lakini zinaweza kuhuishwa, na zinaweza kubadilishwa ili kupata hatimiliki kamili, baada ya maeneo husika kupimwa.

Katika Wilaya ya Mbozi, vijiji vingi vimepatiwa hatimiliki za kumiliki ardhi za vijijini na baadhi ya watu wenye hakimiliki za kimila wamepata hatimiliki. Wizara ya ardhi imeruhusiwa kupanua mchakato huu wa kumilikisha ardhi kwa wilaya zingine 30 na miji mingine.

Mipango Miji katika jiji la Dar es Salaam itapitiwa upya mwaka 2007. Hii itaweza kurahisisha kupata fursa ya kuhalalisha biashara (zikiwemo biashara ndogo).

Mpango wa Marekebisho ya Serikali za Mitaa zinazoendeshwa na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika ofisi ya Waziri Mkuu inakazi ya kuzifanya Serikali za Mitaa zijiendeshe kwa ufanisi na uwajibikaji. Hii ni pamoja na kutoa ushauri wa mabadiliko yoyote kwa shughuli za watendaji wa Serikali za Mitaa sanjari na utoaji mafunzo kwa watu mbalimbali za maafisa wa serikali za Mitaa kufuatana na tofauti zao za kiutendaji.

Mabadiliko yoyote ya kazi au programu za mafunzo na maendeleo ya Maafisa wa Serikali za Mitaa (kama vile yale yanayohitajika kwa ajili ya marekebisho ya MKURABITA) yatahitajika kuchanganywa ndani ya kazi na programu za Marekebisho ya Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa.

Serikali iepuke kuanzisha asasi mpya na zenye gharama kubwa bila sababu. Hata hivyo, baadhi ya marekebisho yanayopendekezwa yanaweza yakahitaji kiwango fulani cha uratibu ambao ni mgumu sana au utakaotumia muda mwingi kiasi kwamba asasi zilizopo zikashindwa kumudu. Hali ya namna hiyo inahalalisha kuanzisha asasi mpya kwa gharama za ziada. Kwa mfano:

- Taasisi mpya kwa ajili ya kusimamia mchakato wa kuunda mfumo mmoja, unaoratibiwa wa masjala za mikataba na makubaliano ya ardhi, biashara na masuala mengine, na kwa ajili ya kuunganisha mfumo huo

katika vyanzo vingine vya habari kama vile mfumo mmoja wa usajili wa biashara na habari za biashara

- Taasisi mpya ya kuongoza mchakato wote wa kurasimisha ardhi ya vijijini na mijini iliyokodishwa.

Kumekuwa na majadiliano fulani kuhusu kuanzishwa kwa **Mamlaka kuu** ya Kurasimisha Mali na Biashara ili kusimamia utekelezaji wa mageuzi yote ambayo yamependekezwa. Pendekezo linalohusiana na hili ni lile la kuanzisha ‘Sera ya Taifa kuhusu Uwezeshaji wa Wajasiriamali’ kama njia ya cha kuwasaidia wajasiriamali wa sekta isiyo rasmi katika kuendesha biashara kwa faida kwenye sekta rasmi. Serikali iamue kama mamlaka mpya ni muhimu, au marekebisho yanaweza kusimamiwa na vyombo vya dola vilivyopo. Labda swali muhimu ni: je kutakuwa na mkabala mpya wa uwezeshaji wa kiuchumi ambayo ni tofauti na muhimu sana kisiasa kiasi kwamba utahitaji asasi mpya kwa ajili ya kuhakikisha kuwa asasi nyingine za kiserikali zinautekeleza ipasavyo?



Sehemu ya Pili: Maswali kuhusu MKURABITA

Kama tulivyoona katika Sehemu ya 1, MKURABITA ni seti kubwa na tata ya mapendekezo, yenye shabaha ya kuongeza ushiriki wa watu maskini kwenye uchumi rasmi wa Tanzania. Kimsingi, programu hii inakusudia kuwashawishi watu maskini kuandikisha na kusajili ardhi, mali na biashara zao. Mara urasimishaji utakapokuwa umefanyika, watu maskini watakuwa na fursa ya kutumia mali yao kama dhamana kwa mikopo ili kupanua biashara zao na kuboresha maisha yao.

Mchakato wa urasimishaji pekee utahusisha marekebisho makubwa ya mfumo wa kisheria na kiutawala ili kuufanya uweze kuwahudumia Watanzania wa kawaida katika hali watakayoimudu. Mapendekezo yatakayotolewa ili kufanikisha lengo hili lazima yazingatie masuala mengi, kama vile jinsi ya kuoanisha sheria za kimila na utaratibu wa mfumo rasmi wa kisheria na jinsi ya kuhakikisha kuwa benki zitatoa mikopo kwa watu maskini zaidi mara watakapokuwa na hatimiliki za mali zao. Hata hivyo, pia tumejifunza kuwa masuala mengi lazima yaangaliwe kabla watu maskini hawajaweza kutumia fursa hii. Stadi za Biashara lazima ziboreshwe na watu wengi watahitaji pia kupatiwa mafunzo kuhusu utunzaji wa hesabu na kodi ili waweze kutimiza majukumu yao katika uchumi rasmi.

Mapendekezo ya MKURABITA bado hayajakamilika. Serikali na Bunge la Tanzania zitafanya maamuzi ya mwisho kuhusu mapendekezo yapi yatekelezwe. Kabla ya maamuzi haya kufanyika, Watanzania wanayo haki ya kujua mapendekezo yatawaathiri kwa namna gani katika maisha yao ya kila siku. Kwa sababu hii ni muhimu watu wengi iwezekanavyo wajue kuhusu MKURABITA na waweze kukubali au kukataa mapendekezo yake kwa njia ya uelewa.

Tayari watu wengi wameshatoa maoni yao kuhusu MKURABITA. Hawa ni pamoja na wawakilishi wa maeneo mengi ya jamii ya Watanzania, wanataaluma, vyama vya kijamii, wanasheria, wakulima, wafugaji, wafanyabiashara na viongozi wa serikali. Watu mbalimbali wana viwango mbalimbali vya uelewa wa mapendekezo. Watu wengi wanajua kidogo kuhusu programu hii, lakini wachache sana wanajua kila jambo lililo ndani yake. Baadhi ya watu wanakubali baadhi ya mapendekezo na kupinga mengine. Baadhi ya watu wanaiona programu hii kama wazo zuri endapo mapendekezo yake yote yatatekelezwa kikamilifu na haki za Watanzania maskini zaidi zikilindwa wakati wote. Wengine wanafikiri kuwa MKURABITA unaweza kuleta manufaa makubwa kwa wale ambao wana mali tayari na kuongeza tofauti za kipato.

Watu wengi wameuliza maswali kuhusu namna ambavyo programu itatekelezwa na iwapo itaboresha maisha ya watu maskini zaidi nchini Tanzania. Katika sehemu hii tutaangalia baadhi ya maswali hayo. Maswali mengi hayana majibu rahisi. Hii ni kwa sababu mara nyingi ni vigumu kutabiri kutatokea nini mapendekezo yatakapotekelezwa. Maswali na majibu tutakayoangalia hapa ni muhtasari wa yale watu mbalimbali wanayofikiri yatatokea.

SW 1. Urasimishaji wa mali umesaidia kupunguza umaskini katika nchi nyingine zinazoendelea?



Nchi chache sana zinazoendelea zimetokeleza programu za urasimishaji mali kama ilivyopendekezwa chini ya MKURABITA. Ushahidi uliopo mpaka sasa unaonyesha kuwa watu maskini wanataka kupata hatimiliki za mali zao ili kupata usalama katika umiliki wao. Hata hivyo, watu wachache sana, na hasa wale ambao ni maskini zaidi, wanachukua mikopo kulingana na thamani ya mali zao. Hii inaweza kuwa kwa sababu watu maskini sana hawataki kuwa katika hatari ya kupoteza nyumba zao au biashara ndogondogo kutokana na kushindwa kurejesha mkopo. Wanapendelea kutumia vyanzo visivyo rasmi vya mikopo kwa kutegemea uhusiano binafsi wa kijamii.

SW 2. Je, ni nani atanufaika zaidi na MKURABITA?



Lengo la MKURABITA ni kupunguza umaskini kwa kuwasaidia watu maskini kupata mikopo. Hata hivyo, baadhi wamependekeza kuwa matajiri, ambao wanaweza kumudu hatari inayohusiana na kutumia mali kama dhamana ya mkopo, ndio wanaoweza kunufaika zaidi na programu ya kutoa hatimiliki. Kama hili ni kweli, basi tofauti kati ya matajiri na maskini inaweza kuongezeka nchini Tanzania kwa kuwa wale ambao wanaweza kumudu kuwekeza na kutojali hatari watapata faida za vitegauchumi hivyo, wakati wale ambao hawawezi kujiingiza katika hatari wataendelea kuwa maskini zaidi.


Kumbuka:

Baadhi wanapendekeza kuwa haiwezekani kufikia maendeleo ya muda mrefu nchini bila kuongeza kwanza viwango vya tofauti za kipato. Watu wa kwanza kunufaika na kukua kwa uchumi ni wale ambao huwekeza bila woga wa kupata hasara. Kama watu hawa ni wale ambao wana mali nyingi zaidi za kuanzia basi wana uwezekano wa kuwa matajiri zaidi kuliko wale ambao wanaogopa kupata hasara. Hata hivyo, imeelezwa kuwa muda unavyopita faida za kukua kwa uchumi zitaonekana katika ngazi zote za jamii, hata kwa wale maskini zaidi. Wewe unaonaje?

Ili kuwashawishi watu maskini waweze kuwekeza, MKURABITA inapendekeza kuwa wapatiwe mafunzo ya biashara na kwamba kanuni na taratibu za biashara zirahisishwe na zilingane pote. Ni muhimu kuhakikisha kuwa mafunzo hayo yanaendana na mahitaji ya Watanzania wa kawaida na kuwa yatatolewa kwa kila mtu anayehitaji, ili manufaa ya urasimishaji yapatikane katika ngazi zote za jamii.

Mpaka sasa, programu za mafunzo zinazosaidiwa na serikalii zimekuwa na ukomo kulingana na mahitaji, na zimekuwa zikifanyika sana mijini. Uzoefu unaonesha kuwa kufikia mahitaji ya mafunzo na ushauri inahitajika kiasi kikubwa cha fedha, mipangilio na ushirikiano baina ya watoa huduma wa serikali na wasio wa serikali.

Serikali tayari ina Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Tanzania, MKUMBITA. Kwa sasa hatujui jinsi ambavyo MKURABITA na MKUMBITA zitafanya kazi kwa pamoja. Ili kutimiza mahitaji ya watu maskini kuna haja ya kulenga miradi midogomidogo.



SW 3. Je, mikopo zaidi itasababisha kukua kwa uchumi?



Hii itategemea ni marekebisho gani yamechaguliwa, na kwa namna gani yanatekelezwa vizuri, na yanatumikaje. Mtu anaweza kujiuliza kwa mfano, kama itakuwa rahisi kwangu kuisajili biashara yangu na kukopa fedha, je nitawekeza fedha hiyo katika biashara yangu kwa faida? Hivyo, kama fedha zilizokopwa zitawekezwa kwenye bidhaa za kibiashara au kutoa huduma, basi nafasi za ajira zitakuwa imeundwa na baadhi ya faida zitaenda kwa watu maskini. Kama mkopo utakuwa umepatikana kwa dhamana ya kiwanja kitupu ili kugharamia ujenzi wa nyumba kwenye kiwanja hicho basi fedha hizo zitawanufaisha wale wanaofanya kazi ya ujenzi na kampuni zinazosambaza vifaa vya ujenzi kama vile saruji na vifaa vingine. Hata hivyo, kama mtu atatumia fedha alizokopa kununua nyumba nyingine ili kuikodisha kwa wapangaji basi uchumi hautanufaika kwa kuwa hakuna kitu kilichozalishwa.

SW 4. Je, thamani ya ardhi na nyumba yangu itaongezeka, na nitapata faida au hasara?



Kama ni vigumu sana kuuza au kuhamisha umiliki wa mali, basi mali hiyo ina thamani ndogo kifedha. Lakini hii haina maana kuwa haina thamani. Kama nyumba inaipatia familia mahali pa kuishi au njia ya kuendesha maisha yao basi ina thamani kubwa kwa familia hiyo.

Lakini, kama familia imeandikisha na kusajili ardhi au biashara yao basi watakuwa wamejiwekea umiliki salama na unaoweza kuhamishika kisheria. Kukiwa na aina hii ya umiliki mali inaweza kuuzwa kwa wanunuzi wengi wa uhakika. Hata hivyo, kama mali ipo maeneo ya ndani vijijini inawezekana kusiwe na watu wengi watakaotaka kuinunua mali hiyo hivyo thamani yake kifedha haitaongezeka. Kwa upande mwingine, kama mtu atarasimisha mali mahali ambapo pana uwezekano wa kuendelezwa basi thamani yake inaweza kuongezeka.

Iwapo umepata hati ya nyumba yako iliyoko eneo ambalo halijapimwa, thamani ya nyumba yako inaweza kupanda litakapopimwa. Je hali hii itaathiri utajiri wako? Inawezekana, endapo tu utaweza kuitumia nyumba hiyo kama dhamana ya mkopo. Kama utaiuza hiyo nyumba, utahitajika kulipa zaidi ili upate nyumba nyingine yenye hati miliki.

SW 5. Je nitanufaika kwa kusajili na kupata leseni ya biashara yangu?



Biashara rasmi (iliyosajiliwa na kupatiwa leseni, na yenye mali zilizotambuliwa, mahesabu safi, kumbukumbu za kodi na eneo halali) itakuwa yenye manufaa zaidi kuliko biashara isiyo rasmi. Ni dhahiri kabisa itakuwa rahisi kwa biashara aina hiyo kupata mkopo kutoka benki. Hata hivyo, thamani ya biashara nyingi ndogo, inategemea stadi, uwezo na mawasiliano ya watu wanaoziendesha. Kwa mfano fundi umeme anaweza kufanya kazi zake nyumbani, akiwa na vifaa vichache. Ukimtoa fundi huyu, biashara hii haina thamani. Vivyo hivyo kwa biashara zingine nyingi zinazoendeshwa na watu binafsi, familia au vikundi. Kwa biashara za aina hiyo, MKURABITA utarahisisha zifanyike rasmi na kupata huduma za fedha na nginginezo, hata kama biashara haiuziki.

Taasisi ya Uhuru na Demokrasia – ILD, imependekeza aina 2 za muundo wa asasi za biashara, aina zote hizi, zinahusisha ukomo wa umiliki, ambao unahitaji kutofautisha kabisa mali ya mwenye biashara na ile biashara yenyewe. Ki utendaji, hii inaweza kuleta matatizo kwa wafanyabiashara wengi wadogo, kwa kuwa ni muhimu kwao kuweza kuhamisha vifaa na fedha kati ya nyumbani na biashara. Fundi selemara anaweza kutumia baiskeli yake kwenda sehemu yake ya kazi na mwanafamilia wake pia anaweza kutumia baiskeli hiyo hiyo kwendea sokoni. Watu wanaofanya biashara kama kikundi (kama washirika) wanaweza kusaidiwa zaidi wakarasisiwa kuanzisha na kusajili ushirika rahisi wa kibiashara usio na ukomo wa mali.

SW 6. Je kila mmoja anayerasimisha mali yake ataweza kupata mkopo?



Watu wenye hatimiliki halali kisheria za mali ambazo umiliki wake unaweza kuhamishwa kwenda kwa mwingine au shirika jingine wanaweza kupata mikopo kwa urahisi. Hata hivyo, kuna sababu kadhaa zinazosababisha watu wenye hatimiliki kupata ugumu wa kupata mkopo baada ya urasimishaji.

Kwanza, mali ambayo ina hatimiliki inaweza kuwa na thamani ndogo kifedha. Kama kiwanja au shamba ni kidogo na kipo vijijini, thamani yake kifedha inaweza kuwa ndogo sana. Kwa hali hii, benki inaweza kukataa kutoa mkopo kwa kuwa mkopo utakuwa mdogo sana na, kama mtu anayetaka mkopo akishindwa kurejesha, benki pia inaweza kuwa na matatizo ya kuuza mali hiyo. Jamii ilipo mali hiyo inaweza kuamua kupinga kuuzwa kwa kiwanja hicho na kufanya iwe vigumu kukiuzwa. Kwa vile watu wengi maskini sana Tanzania wana viwanja vidogo vijijini inawezekana kuwa wengi bado watapata ugumu wa kupata mikopo baada ya urasimishaji.

Hata hivyo, kuna uwezekano kuwa wakopeshaji wadogo, kama vile vyama vya akiba na mikopo (SACCOS), wanaweza kuwakopesha watu wenye hatimiliki za mali zao. Katika miaka michache iliyopita jijini Dar es Salaam, watu wengi wameomba na kupata hati za nyumba, ambazo zinatumiwa kwa miaka miwili na zinaweza kurudia kuongezewa muda. Baadhi ya asasi za kifedha zimetoa mikopo kwa watu hawa kwa msingi wa kutambua umiliki wake.

Pili, kwa suala la mikopo kwa ajili ya biashara, benki itakopesha fedha kama inafikiri mtu anayeendesha biashara ana mipango mizuri ya kurejesha mkopo bila kupoteza mali yake.



SW 7. Je biashara ndogondogo mijini inabidi zihamishiwe mahali fulani kabla ya kurasimishwa?



Kuna pendekezo katika MKURABITA kuwa waendesha biashara ndogondogo zisizo rasmi wapewe maeneo ya kufanyia biashara. Haya yanatakiwa yawe mchanganyiko wa viwanja maalum na maeneo ya jamii. Kama ni mpango wa mkakati wa ushirikishwaji wa maendeleo ya miji, wafanyabiashara ndogondogo na wengine walitakiwa washirikishwe katika kuchagua maeneo.

Kama viwanja maalum vya biashara vinavyohusika, MKURABITA hauko wazi kama viwanja hivi vitakuwa vitagawanywa katika maeneo ya masoko makubwa mahali fulani au kama vitagawanywa kwa usawa katika maeneo ya mjini. Wafanyabiashara wadogo watahitaji kushiriki katika mchakato wa kupanga mipango ili kuhakikisha kuwa mahitaji yao yanazingatiwa. Watu wengi watakuwa wamesikia kuwa wafanyabiashara wadogo katika baadhi ya maeneo ya mjini wameshamishwa kutoka barabarani kwenda kwenye maeneo ya masoko. Baadhi ya wafanyabiashara hawa wamelalamika kuwa ni vigumu zaidi kwao kuzalisha mapato katika masoko haya. Baadhi ya watu wamependekeza mipango miji itoe nafasi ya matumizi mchanganyiko ya ardhi katika maeneo husika. Kwa maneno mengine, kila eneo liwe na mchanganyiko wa nyumba, maduka na viwanda vidogovidogo. Kwa njia hii, biashara ndogondogo zinaweza kuwa karibu na wateja wao badala ya kuwa kwenye masoko makubwa, ambayo yanaweza kuwa vigumu kufikiwa na baadhi ya watu.

SW 8. Je kiwanja kidogo kitatolewa hati kisheria?



Suala la ukubwa wa chini wa kiwanja kidogo ambacho kitapatiwa hatimiliki ni muhimu kwa watu maskini. Ni muhimu zaidi katika maeneo ya mijini na vijijini ambapo kuna utamaduni wa kugawa ardhi kwa ajili ya matumizi ya kizazi kijacho.

Kanuni za Mpango Miji na Nchi (Viwango vya Nafasi) za 1997 zinasema kuwa viwanja visiwe vidogo zaidi ya mita za mraba 400. Katika maeneo ya mjini, watu wachache sana watamudu kununua viwanja vya ukubwa huu. Pia, kama kanuni hizi zikitekelezwa wakati ardhi inapotolewa hatimiliki maeneo ya mjini, viwanja vingi havitakuwa vikubwa kiasi cha kutosha kustahili kutolewa hatimiliki. Viwanja vingi katika maeneo ya mijini vina ukubwa wa eneo kati ya mita za mraba 100 na 300 na asilimia ndogo tu vinazidi mita za mraba 400, na maeneo mengi hayazidi mita za mraba 100.

MKURABITA hautoi mapendekezo yoyote kuhusu ukubwa wa chini wa kiwanja kwa ajili ya kutolewa hatimiliki, lakini ni wazi kwamba utekelezaji wa kanuni zilizopo utakuwa na maana kuwa watu maskini zaidi watatengwa katika mchakato wa utoaji wa hatimiliki. Ili MKURABITA utimize malengo yake ya kurasimisha mali za watu maskini itakuwa vizuri kuangalia kanuni zilizopo na kufanya mabadiliko.

SW 9. Haki za wanawake na familia zitalindwaje wakati wa urasimishaji?




Katika sheria nyingi za kimila mali huwekwa katika jina la mwanaume mkuu wa familia. Moja ya matatizo makubwa kuhusu urasimishaji ni kuwa sheria hii itaimarisha umiliki wa ardhi kwa wanaume.

MKURABITA unatoa maoni kidogo kuhusu ulinzi wa haki za wanawake na familia zaidi ya kusema kuwa kanuni za sasa kuhusu ushiriki wa wanawake katika miamala ya mali zifuatwe. Kwa sasa, wanawake wana haki ya kueleza kukubali kwao katika uzaji wa mali.

Suala jingine ambalo lazima liangaliwe ni lile la ndoa zisizo za kisheria. Hizi zinaweza kutambuliwa chini ya sheria za kimila lakini zinaweza zisitambuliwa chini ya mfumo mmoja unaokubalika kisheria. Pia kuna haki za watoto waliozaliwa katika ndoa ambazo hazina budi kuzingatiwa. Haki za wanawake na familia katika utamaduni wa ndoa za mitala pia lazima zifafanuliwe.

Ili kuhakikisha kuwa haki za wanawake na familia zinalindwa kikamilifu katika kumiliki mali ni vizuri kuandaa mazingira ambapo wanafamilia wote watakuwa wakijua haki hizi na waweze kushiriki kikamilifu katika kutoa maamuzi kuhusu masuala yanayohusu mali. Mabadiliko ya mtazamo yanatakiwa.

Kitu gani kingine ambacho MKURABITA inaweza kufanya ili kulinda haki ya mwanamke na mtoto?



SW 10. Utoaji wa hatimiliki za ardhi vijijini utafanyika kiusawa?



Moja ya changamoto kubwa zinazokabili MKURABITA ni jinsi ya kuhakikisha kuwa mipango, upimaji na utoaji wa hatimiliki za ardhi unafanyika kwa ufanisi na kwa usawa katika ngazi za maeneo husika. Swali moja la muhimu ni: Je Serikali inapaswa kuanzisha kampeni ya nchi nzima ya kupima na kutoa hati kwa viwanja binafsi vya ardhi ya vijijini? Hivi sasa kama unamiliki ardhi kimila, au unataka kununua hatimiliki kutoka kwa mtu fulani, unaweza kulipia upimaji na kuomba hatimiliki. Hata hivyo, gharama ya upimaji kwa mtu binafsi, ni ghali na inaweza kufanyika njama baina ya viongozi wa vijiji na watu wengine kutoka nje ya kijiji au matajiri bila jamii hapo kijijini kufahamu. MKURABITA unatazama jinsi gani Serikali za Mitaa zinaweza kupima viwanja vyote (au baadhi) Kijijini, na kutoa hati kwa viwanja hivyo kwa wakati mmoja. Hii ni rahisi zaidi, na watu watatambua kuwa kuna kitu kinafanyika! Hata hivyo inaweza kuleta uvamizi wa ardhi. Kwa nini? Kwa sababu watu watahisi kuwa huenda ikawa nafasi yao ya mwisho kupata ardhi zaidi kwao na kwa vijiji vyao. Kwa njia hii, kuna hatari kuwa watu wenye nguvu zaidi ndani ya jamii watapata ardhi dhidi ya wale wasioweza kudai haki zao za kumiliki ardhi kama vile wanawake, watumiaji ardhi wa kawaida, na vizazi vijavyo vina hatari zaidi ya kukosa ardhi endapo yote imepatiwa hatimiliki.

Iwapo ardhi imepewa hati miliki kwa wakati mmoja au kulingana na mahitaji, ni kwa vipi utoaji hati miliki unaweza kufanyika kwa urahisi na kwa gharama nafuu? Pendekezo moja, la MKURABITA ni kwamba badala ya kutegemea Maafisa Wilaya, Maafisa vijiji na watu waelimishwe kuendesha mipango shirikishi ya matumizi ya ardhi kwenye maeneo yao. Ili jamii ipate nafasi ya kujadili jinsi ya kugawana ardhi. Viongozi hao pia wapatiwe mafunzo ya kuendesha upimaji wa viwanja, kutumia njia ya vifaa vya kielektroniki katika kupima ardhi ijulikanayo kama “Global Positioning System – GPS). Hii ingeweza kuongeza kasi ya mchakato. Unadhani itafaa?

Endapo sehemu kubwa ya ardhi vijijini na mijini inapatiwa hati miliki kwa wakati mmoja, kama MKURABITA unavyopendekeza, kunaweza kutokea migogoro, ya zamani na mipya, inayohitaji kutatuliwa ndani ya muda mfupi. Hii inaweza kutendeka kwa haki? Pendekezo la MKURABITA ni kuboresha stadi za usuluhishi miongoni mwa kamati au mabaraza ya ardhi vijijini na mabaraza ya watu kupitia mafunzo, kuwapatia nyaraka zinazokubalika kwa ajili ya kurekodi makubaliano yaliyofikiwa na kanuni madhubuti za kutumika katika masijala za vijijini na wilayani. Kama mgogoro hauwezi kutatuliwa ndani ya eneo husika, MKURABITA unapendekeza kuwa mamlaka za wilaya ziteue msuluhishi na kuomba utoaji wa hati miliki kuendelea katika maeneo yasiyo na migogoro.

Katika kuhakikisha haki inatendeka ni lazima wakazi wote waarifiwe kwa wakati muafaka kuhusu kuwepo kwa mikutano ya hadhara kijijini na wapate fursa ya kuhudhuria.

Umuhimu wa kutenda haki katika mchakato wa utoaji hatimiliki usipuuzwe kwani unahusu maisha na maendeleo ya jamii nchini pote. Watu wachache wenye uwezo wa kumiliki mali ndani na nje ya jumuiya kamwe wasiachiwe kutumia nafasi za mchakato wa kutoa hatimiliki kujinufaisha visivyo halali kwa kuwatumia watu masikini. Watu wengi wanaafiki kuwa, kazi inayohusisha mambo kama mafunzo, kuwasaidia na kuwafuatilia maafisa wa serikali vijijini kwa lengo la kuhakikisha inakuwepo haki katika mchakato mzima wa mipango ya matumizi ya ardhi,

upimaji na utoaji wa hati, ni kubwa na yenye kukabiliwa na changamoto. Hata hivyo, kama mfumo wa haki utaandaliwa utaweza kuwasaidia watu wengi kupata ardhi. Je, unafikiriaje? Unadhani, ni kwa jinsi gani serikali inaweza kuhakikisha kwamba haki ya ardhi inalindwa, na utoaji hatimiliki unafanyika kwa njia za haki?

SW 11. Watu maskini watapataje haki sawa kisheria?



Ili kuhakikisha kuwa watu maskini wanapewa haki katika migogoro inayohusu ardhi au biashara ni muhimu kuwa na utaratibu wa kutatua matatizo ambao unamfikia kila mtu. Migogoro mingi inaweza kusuluhishwa katika ngazi ya mwanzo kwa kutumia taratibu na sheria za kimila, pamoja mfumo wa sheria usio rasmi kama mabaraza ya ardhi ya vijiji na mabara ya kimila ya kata. Mfumo wa mahakama unaweza kuwa ghali kiasi kwamba inakuwa vigumu kwa watu wa kawaida kuutumia, hii ndiyo maana MKURABITA unashauri makubaliano na mashauriano yanatakiwa kuimarishwa na kupanuliwa kwa nchi nzima. Uwezo wa watu wengi wa kupata haki unapunguzwa na kukosa maarifa na uelewa wa sheria na haki zao.

Imependekezwa kuwa, ili kuhakikisha kunatendeka haki katika utekelezaji wa MKURABITA, Watanzania wa kawaida wawezeshwe kujua zaidi sheria zinazoongoza maisha yao na kuwa wawezeshwe kupata haki kwa gharama nafuu. Sheria nchini Tanzania huchapishwa kwa lugha ya Kiingereza, hivyo husababisha ugumu kwa watu wengi kuelewa yale yaliyoandikwa. Kutafsiri sheria na sera kwa Kiswahili na kuzisambaza kupitia kampeni za uhamasishaji za kitaifa kungeboresha viwango vya uelewa wa sheria. Pia imependekezwa kuwa utaratibu wa utetezi wa kisheria wa jamii maskini, msaada wa bure au wa gharama nafuu wa kisheria, unaweza kuboresha utaratibu wa upatikanaji wa haki kwa wale wenye raslimali chache. Hali ya kujenga imani katika mfumo wa kisheria inaweza pia kuboreshwa kwa kurekebisha masuala yenye kugongana kati ya sehemu mbalimbali za sheria. Migongano ya namna hiyo ina madhara kwa haki za watu maskini.

Watu wengi wanakubali kwamba kuanzisha utaratibu mmoja, rasmi wa kisheria ambao utaingiza vipengele vinavyofaa, rahisi na visivyobagua vya sheria ya mila iliyopo inaweza kuwa njia bora zaidi ya kuhakikisha kwamba kunakuwa na upatikanaji sawa wa haki kwa wote.

SW 12. MKURABITA unawahusuje wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi?




Urasimishaji wa ardhi na utoaji wa hatimiliki kwa kawaida huchukuliwa kuwa ni uandikishwaji na usajili wa ardhi kwa mtu au kampuni. Taasisi ya Uhuru na Demokrasia inashauri kwamba, ardhi ya kawaida, kama vile ya misitu, ardhi ya malisho na ardhi ya majosho kwa wafugaji, lazima ibainishwe na ilindwe wakati wa mchakato wa urasimishaji. Hata hivyo, MKURABITA haijaweka bayana ni kwa namna gani hili lingefanyika.

Watu wengi wanahisi kuwa haki ya kimila ya kutumia mali ya Umma ni muhimu zaidi kulindwa kwa ajili ya maisha ya vijijini na inahitaji kulindwa katika mchakato wowote ule unaorasimisha haki za kimila. Thamani ya haki ya ardhi ya jumua

inaweza ikapuuzwa kirahisi. Kwa mfano, watu wengi wanategemea vyanzo vya asili vya maji. Kama mwekezaji atapata hati rasmi ya kumiliki ardhi kwenye eneo lenye chanzo cha maji kinachotumiwa na jamii, matokeo ya hali hii ni lazima yatambuliwe na maandalizi mbadala ya kutosha yafanyike, ikiwemo fidia kamili kwa upotevu wa maisha ambao haukuweza kuzuilika.

Baadhi ya vipengele muhimu vya Ardhi ya Umma vinahitaji kulindwa, kama vile uwezekano wa kuhamisha mifugo kwa mujibu wa ardhi za ranchi, kwamba vinaendelea ufugaji na kuzuia mifugo mingi kuzagaa. Wakati utoaji hati unaendelea vijijini, kunaweza kukawa na shinikizo la kuongeza idadi ya malisho na uhamaji wa wanyama. Hata hivyo, tishio kubwa kwa haki ya Ardhi ya Umma inatokana na ugawaji wa ardhi ya ranchi unaofanywa na serikali kwenda kwa wawekezaji na dola inatumia ardhi hizo kama Hifadhi za Taifa. Baadhi ya watu



wanadhani kuwa kurasimisha haki za Ardhi ya Umma kungeweza kuwalinda kuhusiana na Benki ya ardhi inayoendeshwa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania, ambayo inabainisha wazi ardhi inayoweza kugawiwa kwa wawekezaji, ambayo pia baadhi yake inaweza kuwa ni Ardhi ya Umma inayotumika.

Unadhani urasimishaji huo wa haki za kimila, pamoja na haki za matumizi ya Ardhi ya Umma, kungeweza kulinda haki za Ardhi ya Umma na kupunguza migogoro ya ardhi? Kama ndiyo, haki za kutumia Ardhi ya Umma zifafanuliwe vipi? Na unaweza kufikiria njia ambayo matumizi ya kimila ya Ardhi ya Umma kwa wafugaji na watumiaji wengine kutoka vijijini inavyoweza kurasimishwa?

Maelezo ya 1: Maoni ya wadau kuhusu Faida na Hasara za MKURABITA

Jedwali hapo chini limeorodhesha baadhi ya faida na hatari za MKURABITA kama zilivyobainishwa na washiriki katika warsha ya wadau huko Dar es Salaam mnamo Novemba 2006.

Kupatikana kwa huduma za fedha

Faida Inaweza Kuwa	Hasara Zinazoweza Kuwepo
<ul style="list-style-type: none"> • Upatikanaji zaidi wa mikopo kwa sababu watu watakuwa na nyaraka • Uzalishaji na mapato zaidi kutokana na mikopo • Mapato zaidi kwa Serikali • Ongezeko la thamani kwa mali kwa sababu ya hatimiliki rasmi • Migogoro ya ardhi itapungua kama hatimiliki itakuwa wazi. • Mgawanyo ulio wazi kati ya matumizi ya kijamii na kibiashara 	<ul style="list-style-type: none"> • Mgogoro wa kijamii kutokana na kushindwa kurejesha mkopo – kupiga mnada mali kunaweza kusababisha kusambaratika kwa jamii • Kupoteza mali kutokana na kunyang'anywa • Kutokomeza utamaduni na desturi zilizopo – kwa mfano kufanya iwe ngumu kugawa, hasa kwa watu wengine kuweza kuchukua viwanja vya wengine. • Uwezekano wa watu kutumia mali zao kama dhamana kwa mkopo wa mtu mwingine kwa malipo. • Hatari ya kupoteza ardhi kwenda kwa wageni

Umilikishaji Ardhi - Mijini

Faida Inaweza Kuwa	Hasara Zinazoweza Kuwepo
<ul style="list-style-type: none"> • Uhakika wa kujua una hatimiliki na unaweza kuishi kwenye nyumba yako • Hatimiliki ya mali yako inakupa utambulisho rasmi • Upatikanaji wa mikopo – kwa kupunguza urasimu • Serikali inaweza kuingiza fedha kwa kodi ya mali 	<ul style="list-style-type: none"> • Kama utaratibu wa kutoa hatimiliki si wa wazi na si shirikishi unaweza usiwe na faida • Watu masikini wanaweza kushindwa kurejesha mikopo na kwa hiyo wakapoteza ardhi yao • Hatari ya usimamizi mbovu wa miamala ya usajili wa ardhi • Taratibu zilizorahisishwa pia hurahisisha upokonyaji wa ardhi ya mwingine kwa ulaghai

Umilikishaji Ardhi - Vijijini

Faida Inaweza Kuwa	Hasara Zinazoweza Kuwepo
<ul style="list-style-type: none"> • Kuwa na hati halali, watu watatulia na kuwa wazalishaji zaidi nat watawakeza katika ardhi. Hii ilionakana baada ya Ujamaa Vijijini. • Migogoro ya ardhi itapungua kama hatimiliki itakuwa wazi. • Utoaji hati za viwanja binafsi, au angalau hatua ya mipango ya matumizi ya ardhi hutangulia, utaelekea kulinda maeneo ya umma ndani ya eneo la kijiji. 	<ul style="list-style-type: none"> • Ugawaji wa ardhi hufanya utaratibu uwe mgumu zaidi na kunaweza kuwepo upinzani, k.m. Kilimanjaro, kwa watu wanaweza kuchukulia kuwa hatimiliki haziwezi kugawanyika. • Kwamba umilikishaji utazua migogoro na utaleta wamiliki wa ardhi wasiyo halali • Utaratibu wa kusajili ardhi kwa jina la mwanaume una madhara kwa wanawake. • Gharama za kurasimisha ardhi ya kijijini kwa kutoa hatimiliki ni kubwa. • Wakati ardhi inapowekwa kwa benki ya ardhi katika Kituo cha Uwekezaji Tanzania kwa ajili ya kuwapa wawekezaji, kuna hasara kwamba hakutatolewe fidia ya kutosha. • Kuwa katika mfumo rasmi wa umiliki wa ardhi ina maana ardhi yako italipiwa kodi.

Biashara Vijijini

Faida Inaweza Kuwa	Hatari Zinazoweza Kuwepo
<ul style="list-style-type: none"> • Uwezekano mzuri wa kupata mikopo kwa sababu ya kuwa na hatimiliki • Upatikanaji wa pembejeo za kilimo • Ongezeko la ushindani na kuaminika • Kupungua kwa uhamaji toka vijijini kwenda mijini • Utaratibu wa vijiji ambao hujazia kuongeza ongezeko la thamani 	<ul style="list-style-type: none"> • Inawezekana bei za soko zikashuka kwa sababu watu wengi watakuwa wanapata mikopo na kutoa bidhaa zinazofanana. • Ukosefu wa huduma za ugani na mbinu za ujasiriamali zinaweza kukwamisha watu kutumia fursa • Kunaweza kuwa na mtazamo kuhusu mwelekeo wa kujikimu (wingi) kuliko masoko (ubora).

Biashara Mijini

Faida Inaweza Kuwa	Hatari Zinazoweza Kuwepo
<ul style="list-style-type: none"> Watu watatambuliwa kupitia (leseni na usajili) na hivyo kuwa salama zaidi Serikali itapata kodi zaidi Wafanyabiashara wengi watapata mikopo zaidi Kutakuwa na ongezeko katika uwekezaji kwa vile watatambuliwa Mafanikio muhimu si makubwa katika mpangilio wa biashara za mjini zaidi ya kupata nyumba 	<ul style="list-style-type: none"> Ukosefu wa stadi ya biashara, elimu na ubunifu. Ushindani kutoka kampuni kubwa k.m. Azam na Bakhressa wanatengeneza chapati na kufurika hadi kwa mamantilie, au kuuza barafu mahali ambako wauzaji wasiyo rasmi wamekatazwa Kupoteza mali kama biashara itashindwa baada ya kuchukua mkopo Sheria zinazopingana – k.m. sheria ya 'Nguvu kazi' inayowashawishi watu kuanzisha biashara haiendani na masharti ya mipango miji Biashara ndogo zinaweza kulazimika kulipa kodi haziwezi ambazo hawana uwezo nazo.

Wanawake na Familia

Faida Inaweza Kuwa	Hatari Zinazoweza Kuwepo
<ul style="list-style-type: none"> Programu itawafanya wanawake na vijana watambue zaidi umuhimu wa ardhi Vijana na wanawake wataweza kupata hati miliki. Kutakuwa na fursa ya kupitia upya sheria za kimila na zinazowalinda wanaume Watu watapata ufahamu zaidi kuhusu haki zao –mtazamo wa kihaki 	<ul style="list-style-type: none"> Wanawake na vijana wataathirika kama ardhi itahamishika kirahisi Umilikishaji, usajili na uuzaji wa ardhi unaweza kuleta migogoro ya familia juu ya matumizi yake Kuweka rehani kunaweza kuongeza upoteaji wa umiliki wa ardhi kufuatia kushindwa kurejesha mkopo na itawaumiza wanawake na wategemezi wengine.

Watumiaji wa Ardhi ya Umma

Faida Inaweza Kuwa	Hatari Zinazoweza Kuwepo
<ul style="list-style-type: none"> Chini ya sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 ardhi ya malisho tayari ina kinga kimsingi. Hata hivyo uandikishaji rasmi wa utambuzi wa haki hizo utaimarisha amani na kupunguza migongano. 	<ul style="list-style-type: none"> Mabadiliko katika sheria inayolinda Ardhi ya Umma ambayo haiongezeki thamani ya namna ya matumizi Utoaji wa hatimiliki binafsi unaweza kuzuia mzunguko wa mifugo na kuongeza uharibifu wa maeneo finyu. Hatari ipo ambapo 'ardhi tupu' inkuchukuliwa na Rais

Maelezo ya 2: Marekebisho ya awali

Masuala ya marekebisho ambayo yalitajwa kwenye Sehemu ya Kwanza yametokana na mapendekezo ya Taasisi ya Uhuru na Demokrasia yaliyomo kwenye ripoti yake ya uchunguzi. Hapa tumefupisha vipengele muhimu vya mapendekezo hayo. Katika mpango wake wa hatua nyingine ya ripoti ya uchunguzi, Taasisi ya Uhuru na Demokrasia iliwasilisha mapendekezo kamili 'Marekebisho ya Awali' kwa uchunguzi: hizi pia zimewasilishwa hapa.

Orodha ifuatayo inatoa malezo mafupi ya maeneo muhimu ya marekebisho ambayo Taasisi ya Uhuru na Demokrasia imependekeza yatiliwe maanani katika Awamu ya Sasa ya Marekebisho. Kama utakavyoona, mawazo haya yameingizwa katika mapendekezo yalioorodheshwa kwenye orodha ya kwanza.

Marekebisho ya kuboresha Uongozi wa Umma

- Kuanzisha kanuni za urahisishaji na uboreshaji, sheria, na taratibu za uongozi wa umma, kama vile: kukubali maombi na taarifa za thamani halisi; ugatuaji wa madaraka; kuondoa udhibiti; kuondoa masharti na taratibu zisizo za lazima na zenye gharama kubwa; kuhakikisha kuwa vyombo vya umma vinaweza kupeana habari kwa urahisi; fomu na taratibu sanifu; mfumo wa kuhakikisha wananchi wanapata habari za umma; nk
- Oanisha programu zinazoendelea, miradi na juhudi zilizopo, angalau kwa kiwango fulani, jaribu kuboresha vipengele mahususi vya kiunzi cha kiasasi ili kuwezesha shughuli za ujasiriamali na kutoa hak za kumiliki mali zisizo na dosari nchini Tanzania

Marekebisho ya kuboresha Haki za Kumiliki Mali

- Boresha taratibu zilizopo za urahisishaji kwa kuzingatia, kwa mfano: (a) kuruhusu kazi ya upimaji rasmi ambayo ni ghali na hutumia muda mwingi ifanywe na wataalamu binafsi, (b) kupanga taratibu za usajili ambazo ni rahisi, zilizogatuliwa, zinazofanyika kwa wingi na kwa gharama nafuu kwa kutumia hifadhi data ya kijiografia (c) kupanga taratibu za kisheria za kulinda haki za pande tatu na (d) kuanzisha utaratibu ambao utaepuka kuingiliwa na utawala katika miamala binafsi ya siku zijazo na hivyo kukwepa haja ya idhini ya Halmashauri ya Kijiji
- Anzisha taratibu rahisi, sanifu na za gharama nafuu za usajili wa miamala inayohusu urahisishaji wa majumba na uoanishaji wa usajili wa sasa katika Tanzania bara na Zanzibar

Marekebisho ya kuboresha Fomu za Biashara

- Toa nafasi ya ugawaji mali na upunguzaji hatari kwa kutumia utaratibu wa 'deni ukomo' kwa biashara zote na hasa kwa wafanyabiashara binafsi na washirika
- Anzisha taratibu zilizogatuliwa, rahisi, zilizosanifishwa na za gharama nafuu kwa ajili ya uendeshaji wa biashara zote, na anzisha (a) huduma za ushauri kwa wateja (kuwapatia wafanyabiashara taarifa kuhusu kazi zao, kodi na wajibu mwingine), na (b) kanuni za kufanya ukaguzi na kupunguza maamuzi holela yanayofanywa na wakaguzi

Marekebicho ya kuwezesha uendeshaji biashara katika Soko Pana

- Anzisha taratibu rahisi na za gharama nafuu ambazo zitawawezesha wafanyabiashara binafsi na washirika kuingia mkataba na Serikali ya Tanzania na kufuata masharti ya kisheria na kiutawala kuhusu kusafirisha nje, kuagiza na kutangaza bidhaa
- Unda mfumo wa habari za biashara uliunganika utakaozipatia pande zote husika huduma ya habari iliyo wazi, ya kuaminika na iliyorekebishwa. Mfumo huo, pamoja na habari nyingine, uwe na habari kuhusu: hali ya biashara kisheria; mali zake zinazohamishika na zisizohamishika; rekodi yake ya mwenendo wa kutimiza majukumu ya kibiashara na asasi za kifedha, wateja, wasambazaji binafsi na Serikali; na uwezo wake wa kutimiza majukumu ya kulipa kwa wakati.

Masuala 23 ya Marekebicho ya Awali yalibainishwa na yalipangwa pamoja wenye jedwali kwa kutumia zana tatu za kiuchumi na ngazi tatu za usalama na kuingizwa katika mihimili na safu.

Jedwali: Orodha ya kategoria za Masuala 23 ya Marekebicho ya Awali			
	Kupata haki ya kumiliki mali	Fomu sahihi za biashara	Kupata masoko mapana
Uandikishaji	1. Uandikishaji na usanifu wa mali binafsi na za pamoja	8. Uandikishaji na usanifishaji wa makubaliano binafsi ya kufanya biashara	14. Uandikishaji, usanifishaji na kutekeleza mikataba na dhamana binafsi
Usajili	2. Usajili wa mali 3. Taratibu za kupata na kuhamisha	9. Usajili wa biashara 10. Upatikanaji wa kukubalika kisheria na kuingia katika deni ukomo	15. Mfumo wa habari za kibiashara
Kuingiza Masoko	4. Usajili wa miamala ya majengo 5. Idhini za kujenga, kugawa na kuchanganya majengo 6. Upatikanaji wa habari kuhusu kupanga kanda, matumizi ya ardhi, maeneo yasiyoruhusiwa na maeneo ya umma 7. Kuandaa na kufunga dhamana za majengo	11. Kanuni za msingi za utunzaji wa hesabu 12. Kuzingatia wajibu wa ajira na kodi 13. Ufungaji wa biashara kisheria (kuzuia haki za upande wa tatu)	16. Kupata fedha kutoka pande ya tatu 17. Taratibu za kufanya mikataba ya majengo 18. Taratibu za kusafirisha nje bidhaa na huduma

Masuala mtambuka

19. Uboreshaji wa marekebicho na uainishaji, ikiwa ni pamoja na utaratibu wa kupata taarifa za mrejesho
20. Usuluhishaji wa migogoro (taratibu za mahakamani na nje ya mahakama)
21. Ubainishaji wa watu (vitambulisho na anwani)
22. Upatikanaji wa manufaa ya marekebicho kwa wanawake na vikundi vya wanyonge
23. Upatanishaji wa sheria ya kimila na sheria rasmi

Maelezo ya 3: Maandiko kuhusu MKURABITA

MKURABITA ni mpango endelevu. Utafiti na uchambuzi unaleta mapendekezo ambayo, baada ya mashauriano mapana, yanarekebishwa na kuwa msingi wa utafiti na uchambuzi zaidi. Kupanua polepole mawanda ya ushauri kwa njia hii huhakikisha kuwa (a) njia za kusuluhisha zinabuniwa na (b) kuwa ‘zinamilikiwa’ na wadau mbalimbali.

MKURABITA unalenga kujiainisha na mikakati, programu na miradi mingine ya maendeleo inayoendelea. Hapa tunaorodhesha maandiko ambayo yameandikwa maalum kuhusu MKURABITA

Ripoti ya Tathmini ya Hali Halisi (Oktoba 2005) kurasa 1700 katika juzuu 6

Juzuu la 1	Muhtasari Rasmi (kurasa 25)
Juzuu la 2	Uchumi wa sekta isiyo rasmi Tanzania, muundo na ukubwa wake
Juzuu la 3	Uchambuzi wa asasi na gharama za sekta ya taifa ya sheria
Juzuu la 4	Taarifa za vikwazo vya kutumia mali na kufanya biashara nchini kote
Juzuu la 5	Mtazamo wa hatua kwa hatua wa jinsi Watanzania wa kawaida wanavyoziona taratibu zilizopo za kisheria
Juzuu la 6	Nyaraka zinazosaidia Uchunguzi

Mpango wa Kazi – Hatua ya Muundo wa Marekebisho (Machi 2006) kurasa 109

Ripoti ya Kwanza ya Maendeleo (2006) katika juzuu 5

Kitengo cha Usimamizi wa Programu – Waraka wa Dhana ya Programu – Rasimu ya Mwisho (Februari 2006) kurasa 102

Tume ya Uwezesaji Maskini Kisheria – Makala kuhusu Masuala ya Jumla (Januari 2006) kurasa 24

Ushauri wa Kitaifa kuhusu Uwezesaji Kisheria –Makala 4 za Mada

Vikundi lengwa 7-8 Novemba 2006

Mashauriano ya Kitaifa 29-30 Novemba 2006

- “Upatikanaji wa sheria na utawala wa sheria” – Dr. Fauz Twaib
- “Kufanya haki mali iwanufaishe maskini” – Prof. J M L Kironde
- “Haki za ajira” – Rose Teemba na Cornel Mtaki
- “Kutambua uwezo wa ujasiriamali kwa Maskini katika Tanzania: Matarajio, Changamoto na Kujinasua” – Donath Ulomi.

Maelezo ya 4: Mahusiano kimtandao

Hakikazi Catalyst

Tovuti ya Shirika hili la Kijamii inakuunganisha kwenye maandiko unayoweza kuyasoma (a) sera na programu za serikali za hivi karibuni na (b) tafsiri za nyaraka muhimu mbalimbali kwa lugha rahisi (pamoja na waraka huu)

<http://www.hakikazi.org/>

Tume ya Uwezeshaji Maskini Kisheria

Tume ya Uwezeshaji Maskini Kisheria ni juhudi mpya, huru, za dunia. Inachunguza jinsi mataifa yanavyoweza kupunguza umaskini kupitia marekebisho ambayo yanaongeza kupata ulinzi wa kisheria na fursa kwa wote. Tume inaamini kuwa umaskini unaweza kufutwa tu kama serikali zitawapatia wananchi wote, hasa maskini, vitegauchumi halali kwa kudumisha utawala wa kisheria, kuwapatia watumiaji na haki za kumiliki mali na kinga nyingine za kisheria kama haki kwa wananchi wote badala ya kuwa upendeleo kwa wachache.

<http://legalempowerment.undp.org/>

Taasisi ya Uhuru na Demokrasia (ILD)

Watu bilioni nne katika nchi zinazoendelea na nchi zilizokuwa katika Jumuiya ya nchi za Kisovieti – theluthi mbili ya idadi ya watu duniani – wamefungiwa nje ya uchumi wa dunia: wamelazimishwa kufanya kazi nje ya utawala wa kisheria, hawana utambulisho wa kisheria, hawapati mikopo, hawana mitaji, na hivyo hawana nafasi ya kuendelea. Taasisi ya Uhuru na Demokrasia, iliyo huko Lima, Peru, inapendekeze mkakati kwa marekebisho ya kisheria ambayo yanatoa vitegauchumi kwa watu wengi duniani kwenye uchumi wa soko.

<http://www.ild.org.pe/>

Uangalizi wa Haki za Ardhi

Kikundi cha AZISE zilizochaguliwa (pamoja na NPA) zinaangalia kwa makini shughuli za Tume ya Juu ya Uwezeshaji Maskini Kisheria. Tovuti hii ina sehemu muhimu sana inayokuunganisha kwenye nyaraka husika za Tanzania.

<http://www.landrightswatch.net/>

Jukwaa la Raslimali za Tanzania

Jukwaa la Raslimali za Tanzania ni chama cha kijamii cha kuboresha usimamizi wa maliasili nchini Tanzania kwa kushughulikia masuala ya msingi ya usimamizi wa maliasili. Jukwaa kinatambua kuwa utawala una athari katika namna maliasili zinavyosimamiwa na jinsi zinavyosaidia maisha ya Watanzania. Hivyo Jukwaa kinakusudia kuboresha uwajibikaji, uwazi na uwezeshaji wa wananchi katika usimamizi wa maliasili. Kinafanya haya kwa kuwakutanisha wadau na maslahi mbalimbali ili kupeana habari, kujenga ushirikiano na kushirikiana raslimali kwa lengo moja la kuboresha na kurithisha uongozi na usimamizi wa maliasili. Hivyo Jukwaa ni mchakato wa uhamasishaji na ujenzi wa uwezo, kwa ushirikiano, makubaliano na maslahi ya pamoja.

<http://www.tnrf.org/>

MKURABITA

Tovuti rasmi ya MKURABITA inaandaliwa na inaweza kuanza kutumika mwezi Mei, 2007. Kwa sasa unaweza kupata baadhi ya habari za MKURABITA kwenye Tovuti ya Taifa: www.tanzania.go.tz

Timu ya Wahariri

George Clark - Seafield Research and Development Services

Mark Waite - Norwegian People's Aid

Graham Boyd – Caledonia Centre for Social Development

Emmanuel Kallonga – Hakikazi Catalyst

Philip Connelly – Hakikazi Catalyst

Adam Lingson – Hakikazi Catalyst

Habiba Swedi – Arusha Press Club

Nathan Mpangala – Mchora Katuni

Elaine Mahon - Mshauri

Timu ya Wazalishaji

Hakikazi Catalyst – Uzalishaji na Uwezesaji

Colourprint, Dar Es Salaam - Uchapaji

